# ULINGANISHI WA TABIA ZA WAHUSIKA WAKUU NA DHAMIRA KATIKA RIWAYA ZA KUSADIKIKA NA UTENGANO

**MIZA OMAR MOH'D**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M. A. KISWAHILI - FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

# ITHIBATI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania tasnifu yenye mada: ***“Ulinganishi wa Tabia za Wahusika Wakuu na dhamira katika Riwaya za Kusadikika na Utengano"*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

..........................................................

Dkt. Hadija Jilala

(Msimamizi)

..........................................................

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairusiwi kuiga au kumiliki kwa namna yoyote ile sehemu ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi **Miza Omar Moh'd,** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada yoyote.

…………………………………….

Saini

…………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, Bw. Omar Moh'd Shoka na Bibi Habiba **Hamad Ali** kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunipa moyo katika kipindi chote cha masomo yangu, tangu darasa la kwanza mpaka sasa ninapokamilisha masomo yangu ya Shahada ya Umahiri. Mawazo yao na busara zao katika elimu nitazikumbuka daima na kuwa chachu ya kujiendeleza zaidi.

Aidha, ninaitabaruku kwa wanangu Habiba Abubakar na Haabil Abubakar, pia wakwe zangu Makame Fakih na Dawa Fakih, kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu.

## SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa kila kitu, kwa kunijaalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili na utafiti huu. Namshukuru tena kwa unyenyekevu kwa kusema, *Alhamdulillah Rabbilaalamina*.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati Msimamizi wangu Dkt. Hadija Jilala kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Siku zote, hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa misingi ya nadharia za fasihi, fasihi linganishi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe afya njema na amzidishie kila la kheri, Amin.

Tatu, napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu waliouonyesha kwa kuelewa kuwa nilikuwa masomoni, kwani wakati mwingi waliukosa upendo wa mama. Aidha, napenda kumshukuru kwa dhati mume wangu mpenzi, Dkt. Abubakar Makame, kwa subira, msaada wake wa hali na mali, ushirikiano na ustahamilivu wa hali ya juu aliouonesha katika kipindi chote cha masomo na utafiti huu. Shukrani za pekee kwa ndugu zangu Moh'd O. Moh'd na Said O. Moh'd kwa misaada yao ya hali na mali iliowezesha kutoka kazi hii katika hali ilionayo.

Mwisho, napenda kuwashukuru walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia na vitendo. Walimu hao ni Prof. E. Mbogo, Prof. T. Y. Sengo, na Dkt.  M. Omary. Bila kuwasahau wanafunzi wenzangu wa Shahada ya M. A. Kiswahili wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tawi la Zanzibar kwa ushirikiano wao.

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kulinganisha tabia za wahusika wakuu nadhamira katika riwaya ya Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano*. Pia, malengo mahususi yalikuwa matatu; ambayo ni kueleza muhutasari wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*, kubainisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* na kulinganisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*. Data ya utafiti huu imekusanywa kutoka maktabani na uwandani. Kwa upande wa data za maktabani zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji maandiko na data za uwandani zimekusanywa kwa kutumia mbinu tatu za ukusanyaji data. Mbinu hizo ni majadiliano ya vikundi, usaili na hojaji. Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Uasilia zimetumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa wahusika wakuu katika riwaya zote mbili ya *Kusadikika* na *Utengano*, wamesawiriwa katika tabia za aina mbili; yaani tabia nzuri na tabia mbaya kwa wahusika hao. Pia, waandishi wa riwaya mbili hizi wameathiriwa na mapokeo simulizi ya visakale vya watu wa pwani. Riwaya zote mbili ya *Kusadikika* na *Utengano* zinafanana, sambamba na kutofautiana. Zaidi ya hayo, utafiti huu umebaini kuwa waandishi kwa kiasi kikubwa wanawatumia wahusika wakuu kuwasawiri matendo ya watu katika jamii inayohusika. Wahusika wakuu hao wengine hupambwa kwa tabia nzuri na wengine huvikwa tabia mbaya ili kuakisi tabia za binadamu katika jamii. Mwisho kabisa utafiti huu umetoa hitimisho la jumla na mapendekezo kwa watafiti wengine watakaopenda kuchunguza tabia za wahusika wakuu katika kazi za fasihi.

# YALIYOMO

**ITHIBATI** ........................................................................................................ **ii**

**HAKIMILIKI** ........................................................................................................ **iii**

**TAMKO** ........................................................................................................ **iv**

**TABARUKU** ........................................................................................................ **v**

**SHUKURANI** ........................................................................................................ **vi**

**IKISIRI** ........................................................................................................ **vii**

**YALIYOMO** ........................................................................................................ **viii**

**SURA YA KWANZA** ........................................................................................................ **1**

**UTANGULIZI** ........................................................................................................ **1**

1.1 Utangulizi ........................................................................................................ 1

1.2 Usuli wa Utafiti ........................................................................................................ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........................................................................................................ 3

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................................ 4

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................................................................ 4

1.4.2 Malengo Mahususi ........................................................................................................ 5

1.5 Masuali ya Utafiti ........................................................................................................ 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................................................................ 5

1.7 Mawanda ya Utafiti ........................................................................................................ 6

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ........................................................................................................ 7

1.9 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti ........................................................................................................ 8

1.10 Hitimisho ........ 11

**SURA YA PILI ........ 12**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA ........ 12**

2.1 Utangulizi ........ 12

2.2 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili ........ 12

2.4 Dhana ya Wahusika ........ 15

2.5 Kiunzi cha Nadharia ........ 19

2.5.1 Nadharia ya Uhalisia ........ 19

2.6 Pengo la Utafiti ........ 24

2.7 Hitimisho ........ 24

**SURA YA TATU ........ 26**

**MBINU ZA UTAFITI ........ 26**

3.1 Utangulizi ........ 26

3.2 Eneo la Utafiti ........ 26

3.2.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko ........ 26

3.3 Zana za Utafiti ........ 27

3.3.1 Shajara ........ 27

3.3.2 Kompyuta ........ 28

3.3.3 Simu ya Mkononi ........ 28

3.3.4 Vifaa vya Kunukulia ........ 28

3.4 Uchambuzi wa Data ........ 28

3.5 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti ........ 30

3.6 Hitimisho ........ 32

**SURA YA NNE ......................................................................................... 33**

**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA................................................ 33**

4.1 Utangulizi ......................................................................................... 33

4.2 Muhutasari wa Riwaya ya Teule ..................................................... 33

4.2.1 Muhutasari wa Riwaya ya *Kusadikika* ............................................. 33

4.2.2 Muhutasari wa Riwaya ya Utengano ............................................... 35

4.3 Kubainisha na Kujadili Tabia za Wahusika ...................................... 37

4.3.1 Tabia za Wahusika Wakuu wa Kusadikika ...................................... 37

4.3.1.1 Karama ........................................................................................... 38

4.3.1.2 Majivuno ......................................................................................... 39

4.3.1.3 Wajumbe Sita ................................................................................. 39

4.3.2 Tabia za Wahusika Wakuu wa Utengano ........................................ 41

4.3.2.1 Makusudi ......................................................................................... 41

4.3.2.2 Maimuna .......................................................................................... 42

4.3.2.3 Kazija .............................................................................................. 43

4.3.2.4 Farashuu .......................................................................................... 44

4.3.2.5 Mussa .............................................................................................. 45

4.4 Kulinganisha na Kutafautisha Tabia za Wahusika ........................... 46

4.4.1 Makusudi na Majivuno ..................................................................... 46

4.4.2 Karama na Maimuna ........................................................................ 48

4.4.3 Kazija na Buruhani ........................................................................... 50

4.4.4 Fadhili na Mussa .............................................................................. 51

4.5 Data ya Kuonesha Tabia za Wahusika .............................................. 53

4.6 Dhamira ............................................................................................ 53

4.6.1 Uongozimbaya ... 53
4.6.2 Uzalendo na Ujasiri ... 54
4.6.3 Uonevu na Ukandamizaji (Kukosekana kwa Haki) ... 54
4.7 Dhamira katika Kitabu Cha Utengano ... 54
4.7.1 Nafasi ya Mwanamke ... 54
4.7.2 Uongozi Mbaya ... 55
4.7.3 Usaliti ... 55
4.9 Hitimisho ... 58
**SURA YA TANO ... 59**
**MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 59**
5.1 Utangulizi ... 59
5.2 Muhtasari wa Mjadala ... 59
5.2.1 Kujibu Maswali ya Utafiti ... 61
5.2.2 Mchango wa Utafiti ... 64
5.3 Hitimisho ... 65
5.4 Mapendekezo ... 66
**MAREJEO ... 67**
**KIAMBATANISHO ... 71**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti katika sura hii ya kwanza unahusu utangulizi wa jumla ambao unabainisha vipengele vya awali vya utafiti. Vipengele hivyo ni usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti; lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, mpangilio wa tasnifu, uzingativu wa maadili ya utafiti na hitimisho.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Waandishi mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili (Wamitila, 2002; Ntarangwi, 2004; na Senkoro, 2011) wamechambua wahusika katika kazi za fasihi. Katika kazi zao wataalamu hao wanakubaliana kuwa wahusika katika kazi za fasihi huwa ni viumbe ambao huwakilisha tabia za watu katika jamii.

Kwa mujibu wa Mlacha (1985) wahusika ni watu ambao msanii mwenyewe huwabuni kutokana na maisha ya jamii yake kulingana na kile anachotaka kukifafanua. Kwa upande mwingine, Msokile (1982) anafafanua kuwa wahusika katika kazi yoyote ya sanaa ni watu, wanyama au vitu. Mara nyingi, wahusika hao mwandishi huwasawiri kisanaa ili waweze kuwakilisha nyanja mbalimbali za maisha ya jamii. Waandishi huwasawiri wahusika wao kwa kuwapa sifa pambanuzi ambazo huakisi dhamira maalumu zinazokusudiwa na mwandishi ziifikiye jamii.

Tunapozungumzia kuhusu wahusika mara nyingi tunarejelea viumbe waliopewa sifa ya kutenda kama washiriki katika kazi ya fasihi.. Kama tutakavyoona hapo baadaye kuwa wahusika wamegawanyika katika makundi mawili makuu. Makundi hayo ni

wahusika wakuu wa kazi ya fasihi na wahusika wadogo. Wahusika hao ndio wanaoipamba kazi fasihi na kuifanya iweze kuakisi mambo ya yaliyomo katika jamii (Msokile, 1992). Kwa muktadha huo tabia za wahusika wa kazi ya fasihi ndio ambao husawiri matukio na mambo mbalimbali yanayofanywa katika jamii inayohusika.

Waandishi wa riwaya, nao huwasilisha masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii zao ambayo yanahusu nyanja tofauti za maisha ya wanajamii zao kama vile nyanja za kisiasa, kiuchumi, kielimu, kijamii na kiutamaduni. Pia, wahusika wa aina mbalimbali wamekuwa wakibuniwa katika kazi hizo kulingana na dhamira zinazojitokeza katika riwaya. Kawaida, wahusika huchukuliwa kuwa ndio wanaoijenga riwaya na tabia za wahusika hao ndizo ambazo huibua dhamira. Dhamira ni jumla ya mambo yanajadiliwa katika kazi ya fasihi (senkoro, 1982).

Dhamira za kazi ya fasihi hujitokeza kulingana na matukio ya jamii, wakati, mabadiliko ya jamii na historia ya jamii. Kwa mfano Dhamira zilizoibuliwa kipindi cha ukoloni zililenga kuibua suala la ukoloni na unyonyaji mfano ni riwaya ya kusadikika (1991) ya Shaaban Robert. Dhamira hizi zinatafautiana na dhamira za kazi za sanaa za kipindi cha kipindi baada ya uhuru, ujamaa na kujitegemea ambazo zilijikita katika ujenzi wa jamii mpya. Jamii isiyo na matabaka, uongozi mbaya, ukoloni mambo leo. Dhamira ni kipengele ambacho kinaweza kuhusishwa katika ulinganishaji wa kazi za fasihi. Dhamira hutusaidia kuonesha wasanii wanavyotafautiana katika kuibua matukio ya kijamii kwa tochi ya kisanii. Kwa kulinganisha dhamira za kazi mbali mbali za fasihi, tunaweza kubaini muingiliano na mahusiano ya dhamira kulingana na mazingira na wakati.

Dhamira ya kusadikika.

Dhamira kuu ya muandishi ni ukombozi.Dhamira hii ndio kuu katika riwaya yakusadikika iliyojikita kwenye ukombozi wa kifikra na ukombozi wa kisiasa. Mwandishi mwandishi amemtumia mwandishi karama alieanzisha elimu ya sheria yenye lengo la kuwezesha wananchi ili waweze kushiriki katika mambo mbali mbali ya nchi. Katika kazi za fasihi, wahusika wakuu na wahusika wadogo hujengwa kwa tabia ambazo zinaakisi sifa halisi zinazowakilisha matendo ya binadamu. Kuna wahusika ambao huwakilisha sifa kamili za watu. Wahusika hao hutenda mambo mazuri na mabaya. Hivyo basi, wahusika hao huwa wa aina mbili za tabia; kuna wahusika wenye tabia mzuri ambazo huakisi matendo mazuri yanayowakilisha watu wema na kuna wahusika wenye tabia mbaya ambao huwakilisha watu waovu katika jamii inayohusika (Senkoro, 1982).

Kwa kuwa, wahusika wa aina mbalimbali hujitokeza katika kazi za fasihi na wahusika hao husawiriwa wakiakisi maisha ya wanajamii, hivyo, tumehamasika kufanya utafiti wa kuchunguza tabia za wahusika wakuu katika riwaya za *Kusadikika* ya Shaaban Robert na *Utengano* ya Said Ahmed Mohamed. Hatimaye tumelinganisha tabia za wahusika hao zilizobainishwa na mwandishi mmoja na mwingine ili kuona kufanana na kutofauti kwa wahusika hao.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Wataalamu mbali mbali wamefanya tafiti zinazohusiana na riwaya miongoni mwa wataalamu hao Pamoja na Sengo na Kiango (1973), Senkoro (1977), Mulokozi (1996) na Wamitila (2011). Watafiti wote hawa wamejikita katika kuchunguza masuala ya kifani na kimaudhui pamoja na kusawiri maisha na mazingira halisi ya

jamii lengwa, uchunguzi kuhusu mlingano wa wahusika na dhamira katika fasihi haujachambuliwa kwa kina. Licha ya hali hii bado jamii imekuwa na tatizo la kutokujua kwa undani tabia za wahusika hawa, umuhimu wake pamoja na faida zakekwa jamii yetu. Kwa kuwa kazi za Shaaban Robert zimesawiri na kuakisi moja kwa moja jamii ya Waswahili wa Bara na zile za Said Ahmed Mohamed nazo zimeakisi na kusawiri moja kwa moja tabia na desturi za jamii ya Waswahili wa Zanzibar. Kwa hiyo, mtazamo wa wanafasihi na watafiti walio wengi ni kushughulikia wahusika kwa kuzingatia nafasi zao katika riwaya na si uhusika wao. Kutokana na tatizo hilo mtafiti ameona kuna haja ya kuchunguza kwa kina juu ya uhusika na tabia za wahusika wakuu wa kazi hizi.

Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza tabia za wahusika wakuu katika riwaya za Kiswahili kwa kulinganisha hali inayosimuliwa katika riwaya moja na nyingine. Riwaya za *Kusadikika* (Shaaban, 1951) na *Utengano* (Mohamed, 1980) ni kazi teule ambazo zilichaguliwa kutumika katika utafiti huu. Riwaya hizo zimechaguliwa kwa sababu ndani yake wahusika wakuu wamechorwa wakiwakilisha dhamira tofauti ambazo ni sehemu ya maisha yao.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umejengwa na lengo kuu na malengo mahususi matatu kama inavyojibainisha katika sehemu zifuatazo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kulinganisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano* ili kubaini namna zinavyojenga dhamira.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu umeongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

(i) Kubainisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*.

(ii) Kulinganisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*.

(iii) Kulinganisha dhamira ya mwandishi wa kitabu cha kusadikika na utengano.

## 1.5 Masuali ya Utafiti

Kwa madhumuni ya kufikia malengo mahususi utafiti huu ulijielekeza kujibu maswali yafuatayo:-

(i) Kuna wahusika gani wakuu katika riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* na wamebeba tabia gani?

(ii) Tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* zinafanana na kutofautianaje*?*

(iii) Dhamira zinazojitokeza katika riwaya teule zinalinganaje na kutafautianaje?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawasaidia walimu na wanafunzi wa vyuo, kwani wahusika ni kipengele kimoja wapo cha fani, lakini ndani yake mna mawazo na mambo mengi muhimu yanayowafaa wanafunzi na walimu katika kuwafunza na kujifunza kwao. Pia utafiti huu utawajenga wahakiki katika kukuza uwezo wa uchambuzi na uhakiki wa fani na maudhui katika riwaya ya Shaaban Robert na Said Ahmed. Vilevile, utafiti utachangia katika kupunguza mwanya wa upungufu wa tahakiki za baadhi ya riwaya za Shaaban Robert na Said Ahmed. Miongoni mwa mambo yanayoupa umuhimu wa pekee utafiti huu ni kule kuwa ni mpya na kwamba bado haujafanywa kwa mujibu

wa mipaka ya elimu ya mtafiti. Katika jamii, hususani ile ya waswahili utafiti huu utawasaidia kuweza kufahamu vizuri kazi za Shaaban Robert na Said Ahmed kuanzia fani hadi maudhui yake. Tunaelewa kuwa waandishi hawa bado tungo zao zinapatikana na zina umuhimu mkubwa sana katika jamii yetu. Riwaya zao zinatoa mafunzo mengi na mwamko mkubwa kwa jamii ya waswahili. Mafanikio makubwa yatakayopatikana kwa wasomaji wa utafiti huu yatafungua mioyo na kuamsha fikra za waswahili juu ya utafiti huu.

Halikadhalika, utafiti huu utaweza kutumika kama rejeleo na chachu ya tafiti nyingine za lugha na fasihi. Aidha, utatoa mapendekezo ya tafiti zijazo katika maeneo ambayo utafiti huu haukuweza kuyagusa kutokana na malengo mahususi ya utafiti huu, yatasaidia kuwapa mwongozo watafiti wengine ili kufanya tafiti nyingi zaidi katika lugha na fasihi.

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Kimsingi utafiti huu ulikusudia kulinganisha tabia za wahusika wakuu na dhamira zilizojitokeza katika riwaya za Kiswahili kama ( Kusadikika na Utengano). Kwa hakika uteuzi wa wahusika katika riwaya hizi umefanywa kutokana na wahusika wakuu wa riwaya hizi kujidhihirisha wakiwa wamebeba dhamira mbalimbali zinazoakisi maisha halisi ya jamii zetu hii leo. Hivyo, utafiti huu umelinganisha dhamira za waandishi wa riwaya hizi na uhalisia wake katika jamii. Aidha, utafiti umelinganisha kufanana na kutofautiana kwa waandishi wanaposawiri tabia za wahusika katika riwaya zao. Vile vile kwa upande wa dhamira mtafiti ataangalia dhana ya dhamira na namna zilivyo fanana katika riwaya hizi mbili.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake.

Kwa upande wa mipaka au eneo la mada, utafiti huu umechunguza tabia za wahusika wakuu wa riwaya ya *Utengano* ya Said Ahmed na *Kusadikika* ya Shaban Robert tu. Mtafiti amechagua riwaya mbili hizi kwa sababu kuu moja nayo ni kuwa riwaya hizi zimetungwa na watunzi mahiri sana wa lugha, hivyo ni weledi katika utunzi wa kazi za fasihi katika vipengele vya fani na maudhui. Kwa upande wa mipaka ya eneo la kijiografia utafifi huu umefanywa Zanzibar katika kisiwa cha Unguja.

### 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Kitabu hiki cha tasnifu kina jumla ya sura tano ambazo zimepangiliwa kama ifuatavyo. Sura ya kwanza inabainisha utangulizi wa jumla kuhusu mada ya utafiti kwa kujadili mambo kadhaa. Mambo yanayobainishwa katika sura hiyo ni pamoja na usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, na mawanda ya utafiti. Pia, sura hiyo inaeleza mpangilio mzima wa tasnifu hii na uzingatifu wa maadili wakati wa kufanya utafiti.

Pia, sura ya pili inajadili kazi tangulizi mbalinbali kuhusu tafiti na riwaya ambazo zinaelezea wahusika. Sura inaanza kwa kuelezea historia fupi ya riwaya ya Kiswahili. Pia, sura hii inaelezea dhana ya wahusika na tahakiki za riwaya za Kiswahili, tafiti kuhusu wahusika, kiunzi cha nadharia iliyotuongoza katika kukusanya na kuchambua data za zetu za utafiti, pengo la utafiti na hitimisho la sura.

Halikadhalika, sura ya tatu inahusu mbinu na njia tulizozitumia katika mchakato wa ukusanyaji na uchambuzi wa data hadi kufikia matokeo ya utafiti wetu. Aidha, katika sura hii, tumeeleza eneo la utafiti ambalo data zilizotumika katika utafiti huu zilipatikana na kufanyiwa kazi. Mambo mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, tafiti tangulizi, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data, na hitimisho.

Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Hii ni sura ambayo inaonesha uwasilishaji wa data za utafiti, uchambuzi wa data hizo na mijadala mbalimbali kuhusu na tabia za wahusika wakuu katika riwaya ya Kiswahili nchini Tanzania. Pia, katika sura hii matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa upana wake.

Katika sura ya tano ambayo ndio ya mwisho katika tasnifu hii, hii ni sura inayohusu muhutasari wa mjadala wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo ya mtafiti kwa ajili ya kufanya tafiti zaidi za fasihi ya Kiswahili hususani katika uandishi wa riwaya. Pia, mapendekezo kwa ajili ya tafiti zitakazoendelea katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili Tanzania.

### 1.9 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Padgett (2002), katika utafiti wowote masuala ya maadili hujitokeza na yanapaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Maadili hayo ni pamoja na kuomba ridhaa na kibali cha ruhusa ya kufanya utafiti katika eneo la utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu. Kwa hivyo, sehemu hii inabainisha maadili ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia katika mchakato mzima wa utafiti wake kuanzia wakati wa ukusanyaji wa data ya utafiti na baada ya uchambuzi wa data. Kwa vile, utafiti huu ulihusisha watu kutoka maeneo mbalimbali

na mtafiti kutembelea taasisi mbalimbali za kiserikali na kibinafsi, na kila sehemu ina taratibu zake hivyo mtafiti alipaswa kuzingatia maadili ya utafiti.

Kutokana na sababu hizi, mtafiti kabla ya kuanza kufanya utafiti alitafuta kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kibali ambacho kilimwezesha kupewa kibali kutoka mamlaka inayohusika na utoaji wa vibali vya utafiti kwa upande wa Zanzibar. Kibali kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Zanzibar kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo ya utafiti wake na kumlinda kisheria. Wakati akiwa maeneo yanayohusika mtafiti kabla ya kuwaona watafitiwa aliwaona viongozi wenye mamlaka katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mtafiti alifika kwa masheha wa shehiya ili kujitambulisha kwa kuonesha kibali cha utafiti ili kuwatoa wasiwasi kuhusu uwepo wake na shughuli iliyomsukuma kuwepo hapo.

Pia, baada ya kupata kibali cha kuanza kazi ya utafiti mtafiti aliomba ridhaa kwa washiriki wake bila ya kuwalazimisha na wale waliokataa kushiriki aliwaachia. Pia, watu hao aliwaridhia kwa upole bila ya kuwalazimisha, kwa sababu Kombo na Tromph (2006), wanaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Hivyo basi washiriki wote waliotoa data walifanya hivyo kwa hiari yao. Mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti wake, kuanzia lengo kuu na kwa nini anahitaji data hizo mpaka matarajio yake, ili kupata maoni ya watafitiwa. Baada ya kutoa lengo la utafiti wahojiwa waliuliza maswali ya kutaka ufafanuzi juu tabia za wahusika. Hivyo, mtafiti alitoa maalezo ya kina na watafitiwa wakaridhika juu ya hilo, hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti ambapo wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa uamuzi wao bila kutumia nguvu na mtafiti. Wakati wa kukusanya taarifa mtafiti

aliuliza maswali yake kwa usahihi na kwa sauti ili kufahamika kwa urahisi na kuweka kumbukumbu za taarifa zote katika sehemu inayohusika.

Mtafiti pia, alizingatia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki waliotoa taarifa za utafiti huu kuwa data walizozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na mhojiwa na kutumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Kwa kufanya hivyo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao wakati wa kutoa taarifa ili kulinda siri ya mtoa data. Kwa kulinda ahadi hii ya usiri mtafiti aliyoitoa kwa wahojiwa wake, matokeo yote ya utafiti huu hakuna urejelezi wa jina la mtoa taarifa lilitoandikwa katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Kama wanavyoeleza Kombo na Tromph (2006) kwamba, washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Kwa mantiki hiyo, suala la faragha lilizingatiwa wakati wa ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa. Kwa sababu mtafiti alitambua kuwa kila mshiriki ana haki ya kupata faragha. Watafitiwa wengine walitaka usaili ufanyike majumbani kwao hasa wazee, mtafiti aliamua kuwafuata huko majumbani kwao kwa ajili ya kupata ufaragha na kupata data za uhakika kwani mtafiti alipofuata matakwa ya mtafitiwa aliweza kujisikia kuwa yuko huru na kutoa data za uhakika.

Pia, sayansi ya utafiti umezingatiwa na kufuatwa kabla ya kukusanya data, wakati wa ukusanyaji wa data, baada ya ukusanyaji wa data na katika uchambuzi wa data. Mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu zimezingatia misingi ya kufanya uchunguzi wa sayansi jamii.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza utangulizi wa jumla kuhusu mada ya utafiti, usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti ambayo ndiyo mwongozo wa utafiti huu. Aidha, katika sura ya kwanza tumejadili umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa tasnifu, maadili ya utafiti na hitimisho. Sura inayofuata itaelezea mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inajadili kazi tangulizi mbalinbali kuhusu tafiti na riwaya ambazo zinaelezea wahusika. Sura inaanza kwa kuelezea historia fupi ya riwaya ya Kiswahili. Pia, sura hii inaelezea dhana ya wahusika na tahakiki za riwaya za Kiswahili, tafiti kuhusu wahusika, kiunzi cha nadharia, pengo la utafiti na hitimisho la sura.

## 2.2 Historia Fupi ya Riwaya ya Kiswahili

Baadhi ya wataalamu na waandishi wa fasihi ambao wametafiti kazi mbalimbali za riwaya za Kiswahili na hata riwaya za kigeni. Baadhi ya kazi tangulizi ambazo tumezipitia kuhusu tafiti za riwaya za Kiswahili ni kama zinavyoonekana hapa chini. Lakini kabla hatujazijadili kazi hizo ni vyema tuangalie kwa ufupi historia ya riwaya za Kiswahili nchini Tanzania. Historia hiyo inaonekana kama ifuatavyo:

Wakati mwingi fasihi hufungamana na maendeleo ya jamii kwa maana kwamba jamii ndiyo inayoibua na kuendeleza fasihi. Kadri jamii hiyo inavyoendelea katika nyanja mbalimbali za maisha ndivyo tanzu tofauti tofauti za fasihi zinavyojitokeza na kupewa nguvu. Mara nyingi tunaelezwa kuwa chimbuko la riwaya za Kiswahili ni ngano simulizi ambapo wakati wa jioni au usiku wa mapema mababu au mabibi na wajukuu wao walikaa pamoja kusimuliana ngano. Ikiwa huo ndio msingi riwaya andishi za Kiswahili, kama zinavyofahamika siku hizi, zimeingia baada ya ukoloni. Hata hivyo, zina asili katika fasihi simulizi ya jamii za Waswahili kifani na kimaudhui (Njogu & Chimerah, 2008).

Kwa kweli, riwaya za Kiswahili katika kipindi kifupi cha maisha yake zimeweza kupata maendeleo makubwa. Hata hivyo, historia yake ina utata kidogo kuhusu ipi ndiyo riwaya ya kwanza. Ingawa watafiti wengi wanachukulia kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza kipndi cha ukoloni wa Waingereza. Wachunguzi walio wengi wanachukulia kuwa riwaya ya kwanza kabisa ni *Uhuru wa Watumwa* iliyotungwa na James Mbotela mwaka 1934. Kuanzia miaka ya 1950 walijitokeza waandishi mahiri mbalimbali wa riwaya za Kiswahili. Miobgoni mwa waandishi hao ni Shaaban Robert aliyeandika riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Adili na Nduguze* (1952). Pia, katika miaka ya 1960, Shaaban Robert aliandika riwaya nyingine kama *Utu Bora Mkulima* (1966), *Maisha yangu na baada ya Miaka Hamsini* (1966) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Maudhui makubwa ya riwaya za wakati huo yalihusu zaidi maadili na masuala ya kidini. Pia maudhui yenye kuonesha mivutano iliyokuwepo baina ya watawala wa kikoloni na Waafrika ilibainishwa katika riwaya hizo za awali.

Aidha, riwaya zilizoandikwa kwenye miaka ya 1970 zilijihusisha na maudhui ya ujenzi wa jamii mpya kama vile uongozi na usaliti wa kisiasa; pia, katika kipindi hiki ndicho ambacho inasemekana kuwa riwaya za kisasa ziliibuka. Waandishi wengi chipukizi walijitokeza kuandika riwaya. Miongoni mwao ni Kezilahabi aliyeandika *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), Mohamed Suleiman aliandika *Kiu* (1972), *Nyota ya Rehema* (1978) na *Kivumbi Uwanjani* (1978) na Senkoro aliandika *Mzalendo* (1977).

Katika kipindi cha miaka ya 1980 riwaya za Kiswahili zilianza kuukaribia uhalisia wa kisanaa. Taratibu za maisha kama vile siasa na dini zilianza kutazamwa kwa jicho kali na udhaifu wake ulifichuliwa.

Pia, dhamira kama hizi zilizidi kushamiri katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa kwenye miaka ya 1990 hadi 2000. Katika vipindi hivyo, waandishi mbalimbali wa riwaya wamekuwa wakisawiri dhamira mbalimbali zenye kufichua maovu yaliyomo katika jamii (Mabala, 1993). Riwaya nyingi zilizoandikwa zilijielekeza kwenye dhamira kuu ya ujenzi wa jamii mpya. Kwa sababu baada ya uhuru jamii zetu zimekabiliwa na changamoto mbalimbali katika nyanja zote za maisha kama vile kisiasa, kijamii, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni. Katika uwanja wa kisiasa, kwa mfano, waandishi wamekuwa wakifichua uovu unaofanywa na viongozi wa jamii zetu baada ya kupata uhuru. Baadhi ya riwaya ambazo ziliandikwa miaka ya 1990 ni *Tata za Asumini* (1990) iliyoandikwa na Said A. Mohamed na *Vuta N'kute* (1999) iliyoandikwa na Shafi Adam.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika vipindi mbalimbali zinajibainisha kifani na kimaudhui kiasi kwamba zimeufanya utanzu huu wa fasihi uwe na wapenzi wengi zaidi ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Kwa mfano, katika riwaya hizi miongoni mwao kuna kazi zenye maudhui mazuri ambayo yanajenga jamii kwa kusawiri maisha halisi ya jamii zinazohusika. Wanajamii wanapaswa kuzitumia kazi za fasihi kama kioo cha kujitazamia na kujisahihisha kila ambapo panaonekana kuwa na kasoro. Licha ya hayo, kuna baadhi ya riwaya hususani riwaya pendwa ambazo hujikita moja kwa moja kusawiri dhamira za mapenzi, upelelezi na ujambazi,; dhamira ambazo badala ya kujenga jamii kimaadili, maudhui yake yanaipotosha jamii hiyo. Kupitia riwaya pendwa vijana hupata hamasa ya kujishirikisha na masuala ya ngono, wizi na vitendo vingine ambavyo ni kinyume na maadili ya jamii zetu.

Kwa umla mapitio haya ya kazi za fasihi mbalimali zinaumuhimu mkubwa kwa mtafiti wa kazi hizo, miongoni mwa manufaa hayo ni haya yafuatayo:

(i) Humuwezesha Mtafiti wa kazi za fasihi kuongeza uwelewa wake katika mawanda mapana ya utafiti wake.

(ii) Kugundua mapungufu yaliyojitokeza katika tafiti mbalimbali zilizotangulia.

(iii) Kuweza kujenga uaminifu juu ya tafiti anayoishughulikia Mtafiti wa kazi ya fasihi.

## 2.4 Dhana ya Wahusika

Tunakiri kuwa kazi kadhaa wa kadhaa zimejadili suala la wahusika wakuu na wahusika wasaidizi ingawa hakuna aliyetafiti juu ya tabia za wahusika na jinsi tabia hizo zinavyojenga dhamira. Kwa kuwa utafiti wetu utajikita kwenye wahusika hatuna budi kufasili dhana hii ya wahusika kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, kisha tupitie tafiti tangulizi zihusuzo wahusika.

Wamitila (2003) ameeleza wahusika kuwa ni viumbe hai ambao ni kama mwega au nguzo kuu ya dhamira mbali mbali ndani ya maudhui. Wamitila katika kitabu cha *Uhakiki wa Fasihi* anasema wataalamu waliotangulia sio wataalamu pekee waliojishughulisha na suala la wahusika mitazamo mengine imekuweko miaka kadhaa. Kigezo kimojawapo kimekuwa ni kuangalia nafasi ya muhusika kuhusiana na mgogoro, mtazamo na mwelekeo wa hadithi nzima. Kwa mfano, kazi ya kifasihi huweza kuwa na mhusika anayeuwakilisha mtazamo mzuri na anayechukua nafasi kuu. Huyu ni muhusika nguli au shujaa anayejulikana kama muhusika mkuu. Aghalabu mhusika wa aina hii huwa na kinyume chake, yule ambaye anaupinga

mtazamo wa nguli au shujaa. Huyu huwa hasidi au muwi, tumeona mfano wa wahusika wa aina hii katika riwaya ya Said A. Mohamed ya *Kiza katika Nuru*. Inawezekana kuangalia nafasi anayoishika muhusika katika kazi ya kifasihi kama kigezo kingine. Kuna wahusika ambao watachukua nafasi kuu au wanayoitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho hawa watakuwa ni wahusika wakuu

Njogu na Chimerah (1999) katika kitabu chao *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu* wanaeleza kuwa wahusika wakuu ndio nguzo za rawaya na ndio wanaosheheni hadithi nzima. Ndio wanaoisukuma riwaya mbele kwa sababu matendo na migogoro yote muhimu inayohusu .dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia kwao, na msimamo wa mwandishi kuhusu dhamira, matukio, na vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia kwa matendo na maneno yao. Aidha, mwingiliano wao na wahusika wengine ndiyo mbinu ya kubainisha na kufafanua dhamira kuu.

Mulokozi (1995) katika *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili* anaeleza wahusika wakuu kuwa ni mbabe au nguli shujaa wa riwaya ambaye anasawiri matendo mengi yanayohusu maisha na majaliwa yake. Huyu ni mhusika kiini au mtenzi mkuu katika tanzia za kijadi mbabe aghlabu alikuwa ni mtu wa tabaka la juu ambaye aliangamia kutokana na ama ila au dosari fulani katika tabia au maamuzi yake iliyoitwa *harmatia* kwa kiyunani au *tragic* kwa Kiingereza ama kwa sababu husakamwa na mazingira yanayomzidi uwezo au yote mawili.

Senkoro (2011) anaeleza kuwa wahusika ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu, katika kazi ya fasihi. Katika ngano kwa mfano, kuna matumizi maalum ya wahusika humo tunakutana na wanyama,

wadudu, mimea, mashetani, miungu na viumbe wengine wakiwa ndio wahusika wakuu wa ngano hizo. Aghlabu hadithi fupi na ngano huwachukulia wahusika wake katika kiwango cha jumla jumla cha kuwakilisha tabia na matendo mara kwa mara ya wahusika wa aina hii. Kutokana na jadi ya kimaadili iliyozoeleka katika ngano, hugawanyika katika mafungu makuu mawili. Wahuisika wema na wahusika wabaya wajinga wasioelewa. Tofauti na wahusika wa ngano, wahusika wa riwaya na tamthiliya wanaouchangamano katika tabia na maisha yao. Ni wahusika ambao hata kama katika maisha na tabia zao wanaweza kuwa wawakilishi watu wema au wabaya. Uwakilishi wao ni wenye mapana na marefu nao una mawanda mapana zaidi ya ule wa wahusika wa ngano na wa hadithi fupi fupi. Uchoraji wa riwaya na tamthiliya unawapa wahusika hao uhusika nafsi. Unaoelezwa kwa undani zaidi ya ule wa ngano na wahadithi fupi, na wanaweza kuwa na uzuri, ubaya na ujinga katika maisha yao.

Hata hivyo, uundaji wa wahusika katika riwaya na hata ushairi wa Kiswahili wakati mwingine umeathiriwa na ule wa ngano. Kwa hiyo tunaweza kukutana na wahusika wema wengine wabaya au wajinga. Katika riwaya ya Shaaban Robert *Adili na Nduguze* pia tunakumbana na wahusika wa aina hiyo hiyo. Pia, katika baadhi ya ngonjera za Mathias Mnyampala ambazo aghlabu huwa na wahusika wema wako wa jamaa na wahusika wabaya au wajinga wasio wajamaa, ijapokuwa kwa namna isioaminika, mwishoni mwa kila ngonjera twawaona wahusika wote wakisuluhisha tofauti baina yao kwa mhusika bepari bwanyenye kukubali kuwa mjamaa.

Senkoro (1982) amewagawa wahusika katika makundi makuu matatu. Wahusika wakuu, wahusika wadogo na wahusika bapa. Mtafiti anawaeleza wahusika wakuu

kuwa ni wale ambao wanajitokeza kila mara katika kazi ya fasihi, tangu mwanzo hadi mwisho wa maudhui ya kazi ya fasihi huwa yanamzungumzia na hata kutolewa na mhusika mkuu zaidi ya wahusika wengine. Mara nyingi jambo hili limewafanya wahusika wakuu wa kazi ya fasihi wawe “midomo” ya wasanii wawe vipaza sauti vya watungaji. Wahusika wakuu hasa wa riwaya na tamthiliya huchorwa na wasanii kwa mapana na tabia zao ili kukamilisha unafsi wao. Maelezo yote haya hayamaanishi kuwa ni lazima awepo mhusika mkuu mmoja tu, katika kazi ya fasihi. Hutokea wakawepo wahusika wakuu wawili au hata zaidi wakati mwingine siyo lazima wawepo wahusika wakuu ambao tunawaona katika ubinafsi wao.

Mara nyingi jamii nzima huwakilishwa na muhusika mkuu. Huu ni uhusika wa kiwango cha jamii nzima au kundi kubwa la watu wakati mwingine unamaanisha na tabaka la watu hao. Hivyo, katika kusimamia na kutetea maslahi ya tabaka fulani tunawachukulia watu hao kwa pamoja na kuwaainisha kuwa wote ni wahusika wakuu.

Naye Senkoro (1982) anatoa fasili ya wahusika kuwa ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi ya fasihi. Zaidi ya hapo Senkoro anasisitiza kuwa wahusika wa riwaya ni binadamu inapotokezea kuwa riwaya ina wahusika wasiokuwa binadamu basi riwaya hiyo inateka aina za wahusika wa fasihi simulizi.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996:169) inaeleza wahusika ni watendaji katika kazi ya fasihi. Kwa upande wa fasihi andishi ukiwemo utanzu wa riwaya taasisi inaeleza kuwa wahusika ni binadamu wenye kuwakilisha tabia za kawaida za watu na katika ubinadamu wao wanatafautiana kwa tabia hizo. Taasisi inaendelea kusema kuwa kazi

za wahusika ni kutimiza majukumu ya uhalisia, hapa wanamaanisha kuwa wahusika hutumika kuelezea yale matokeo yalioibuka katika maisha ya watu ya jamii halisi.

Kutokana na mitazamo yote hiyo tuliyoitaja hapo juu tunaweza kujumuisha kwa kusema kuwa mhusika au wahusika wa kazi andishi ni mtu au watu ambao huonekana wakitenda haya na yale ili kuipeleka mbele kiwakati na kimasafa kazi ya fasihi andishi na kuwasilisha maudhui, ujumbe, mafunzo migogoro, msimamo na mitazamo inayohitajika.

## 2.5 Kiunzi cha Nadharia

Hapa tunaeleza nadharia mbalimbali ambazo tumezitumia katika utafiti huu ili kufanikisha lengo kuu la utafiti. Utafiti huu umetumia Nadharia ya Uhalisia na Nadharia ya Uasili.

### 2.5.1 Nadharia ya Uhalisia

Kulingana na Wamitila (2000) Nadharia hii ni mojawapo ya matapo maarufu katika ulimwengu wa fasihi na lenye athari kubwa sana. Dhana ya uhalisia hutumiwa kwa maana mbili kuu. Maana hizo ni kuelezea tapo la kipindi maalum katika fasihi na kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambapo kazi za fasihi zinachukuliwa kama zinavyohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi.

Uchunguzi wa utanzu unaoambatana na uhalisi kwa kiasi kikubwa hauwezi kuzungumzia riwaya bila ya kuyarejelea mawazo yanayohusisha uhalisia. Wanauhalisia hufanya hivi ili kujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi. Kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao na kusawiri kwa kuonesha mandhari na mazingira ya kawaida.

Tapo hili limewekewa msingi na mwanafalsafa anaejulikanwa kama Hegel katika kitabu chake Aesthetik (ujumi).

Kuna faida kubwa tatu zinazopatikana katika matumizi ya tapo hili. Kwanza, ni kusisitiza uainishaji wa maisha ya jamii kupita wahusika kwa uaminifu mkubwa. Pili, mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishaji kwa mambo ambayo yanaonekana katika jamii inayohusika, na tatu hutoa nafasi ya kuyasawiri matukio, mandhari na wahusika ambao huwenda wasiafikiane au wawafikiane na uhalisi wa jamii yake. Mtafiti ameamua kutumia nadharia ya uhalisia baada ya kupitia nadharia mbalimbali na kugundua kuwa kutokana na utafiti wa kazi yake ya kuchunguza tabia za wahusika wa wakuu wa riwaya za Shaaban Robert na Said Ahmed, anatumia zaidi vipengele vya fani na maudhui ili kufikia lengo la utafiti wake.

**FAIDA YA NADHARIA YA UHALISIA**

Miongoni mwa faida ya nadharia hii ni kumfanya mhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi za fasihi (hususan riwaya) Hivyo basi anazingatia saikolojia ya wahusika akatika hadithi. Mhakiki anae zingatia nadharia hii ya uhalisia hupembua namna mtunzi alivyoyadhihirisha uhalisi wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia nawahusika alivyo wasawiri.

**UDHAIFU WA NADHARIA YA UHALISIA**

Udhaifu wa nadharia hii ni kuwa Muandishi anachukulia kua watu wote wana uoni mmoja katika kuyatizama mambo kitu ambacho ni kinyume na uhalisia wa mambo ulivyo.

### 2.4.2 Nadharia ya Uasilia

Kulingana na Bahati Wamitila (2016) nguzo ya nadharia ya uasilia ni maisha kama yalivyokua yaani maisha aslia . Nadharia ya uasilia huchagua maudhui maalum ya kuzingatia. Nadharia ni aina ya ubunifu wa kifasihi ulioendelelezwana kundi la waandishi waliokua na tasnifu maalum ya kifalsafa. Tasnifu hii iliokua zao la maoni iliotokana na mtaalam wa biolojia Charles Darwin katikati ya karne ya 19, ilishikilia kwamba binaadamu alikua chini ya himaya ya maish ya asilia na kamwe hakua na roho (soul) au uhusiano wowote wa kidini uliokiuka kaida za ulimwengu halisi. Hivyo basi binaadamu alichukuliwa kama mnyama wa atabaka la juu ambae tabia mna maisha yake hutegemea uzawa wake na mazingira yake. Ni kwamba binaadamu hurithi tabia zake za kibinafsi pamoja na haja za kiasilia na hua anafuata bila ya hiari, nguvu za kijamii na kiuchumi katika familia, tabaka la kundi alimozaliwa. Waandishi wanaofuata nadharia aghlabu huzingatia masuala asilia ya kisayansi katika maisha huku wakiwasawiri wahusika wao kama walio na nguvu na mivuto ya kinyama kama vile ulafi na hamu kubwa yakufanya mapenzi. Hatima au mwisho wa riwaya za kiasilia huwa ni tanzia.

**UDHAIFU WA NADHARIA**

Miongoni mwa udhaifu wa nadharia hii ni kuchukuliwa binaadamu kama mnyama wa daraja la juu asie yajua mazingira yake, mwenye ulafi nah au ya kufanya mapenzi, hali inayokwenda kinyume na uhalisia wa mambo ambapo si mara zote mwanaadamu atamalizia maisha yake kwa tabu na misukosuko. Kimsingi tunaweza kusema kuwa Uasilia ni aina fulani ya uhalisia. Tofauti kuu inayojitokeza ni kwenye msisitizo wake kwamba uasilia aghlabu unafungwa zaidi kwenye kazi zilizoandikwa

kwenye imani ya kuwa kuna maelezo ya kiasilia ya matukio yote yatukiayo yawe ya kawaida au ya kiroho. Uasilia unaweza kuangaliwa katika viwango viwili vikuu, uteuzi na udhihirishaji. Uteuzi huu ni wa masuala yanayogusiwa au kuzungumziwa ambapo tapo hili linahusu uteuzi fulani wa masuala ya kushughulikia na njia au jinsi maalumu ya kuyashughulikia. Kimsingi dhana ya uasilia hutumiwa kuelezea wasifu maalumu wa kiuteuzi na kiudhihirishaji unaohusishwa na utanzu wa riwaya na ndio msingi mkuu wa matumizi ya dhana ya riwaya ya kimajaribio. Pia huelezea uandishi ambao unaonekana na mwelekeo mkubwa wa kifalsafa au masuala ya kifilosofia. Mwelekeo mkubwa unaoonekana katika kazi za aina hii unaonesha athari kubwa za mawazo ya Darwin kuhusu msukumo wa kibiolojia katika matendo ya kibinadamu. Suala kuu katika mawazo ya Darwin ni kuwa binadamu huishi chini ya mamlaka asilia na hana njia au namna ya kuyakwepa au kuyakiuka mamlaka hayo kiroho au hata kidini. Matendo ya binadamu yanachochewa na nguvu za kiasili. Tunaasema kuwa matendo ya wahusika au binadamu yanahamasishwa na nguvu za kibaolojia.

Kwa kiasi kikubwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya uasilia ujaala ambao unaamini kuwa maisha ya binadamu pamoja na matendo yake vinatawaliwa na nguvu za jaala yake na hawezi kuzizuia. Kwa kutegemea msingi wa maelezo haya tunaweza kusema kuwa uasilia ni uhalisia ambao una vipengele vya kukatisha tamaa Wanauasilia na wanauhalisia wana malengo sawa ya kuusawiri ulimwengu jinsi ulivyo. Tofauti iliopo kati ya mkundi mawili haya ni kuwa uasilia unaelekea kuvimulika visababishi vya hali ya maisha ulimwenguni. Wanauasilia wanaamini visababisha hivyo huwa ni urithi wa kimaumbile pamoja na mazingira. Vipengele hivi kwa maoni yao huathiri tabia na mwazo ya binadamu kwa kiasi kikubwa sana.

Wanauasilia wanaamini kuwa binadamu anazirithi silka fulani ambazo zinaishia kumsukuma kutenda jambo au mambo ambayo vinginevyo asingeyatenda. Baadhi ya silka hizi ambazo huweza kumtawala binadamu katika tabia yake, ni zile zinazohusiana na njaa nia ya kuvichukua au kuvikamata vitu na mapenzi. Zaidi ya silka hizo zenye msukumo mkubwa katika utendaji wa binadamu kuna nguvu nyingine za kijamii na kiuchumi kwenye jamaa, tabaka au mazingira anamojikuta binadamu.

Moore akijadili uasilia wa Kimarekani katika karne ya kumi na tisa anadokeza kuwa riwaya ya kiuasilia huwa na mikinzano au mivutano miwili mikuu. Mikinzano hiyo huhusisha uasilishaji kiumbuji wa tajriba na fasiri ya tajriba inayounganisha dhamira na mtindo wa riwaya yenyewe. Riwaya hiyo humsawiri binadamu kwa namna inavyomuonesha kama kiumbe anayetokeza kutokana na uasilia. Aghlabu wahusika wanaopatikana katika kazi hizi huwa masikini wasiosoma au watu wasioonesha maendeleo ya kiwango kikubwa. Mwanauasilia huimulika sifa ya kishujaa ya wahusika kwa kuwasawiri wahusika wanaohusishwa na jasira ya kishujaa. Riwaya ya kiuasilia na riwaya ya kihalisia hukaribiana na kufanana kwa kuwa zinashughulika na masuala yanayoweza kuhusishwa na wakati fulani uliopo.

Mwanauasilia huwaelezea wahusika wake kama waliotawaliwa na mazingira, urithi kimaumbile, silka. Riwaya au kazi za kiuasilia huwa na hatima au miishio ya msuko wa kitanzia. Mhusika au wahusika wakuu wanasambaratika kutokana na uzito wa misuko suko ya ndani na nje yao. Baadhi ya wahakiki kifasihi wanadai kuwa sifa ya kina cha maelezo katika tapo hili huashirii uhalisi tu bali ni uchunguzi mpevu wa

uhalisi. Inawezekana kuwa ni uasilia haujipambanui na uhalisia kabisa bali huvunja baadhi ya kaida zake tu.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Licha ya kuwa kuna tafiti zilizofanywa kuhusu wahusika wakuu katika fasihi, hadi hivi sasa kazi hizo hazijaziangazia suala la tabia za wahusika wakuu katika riwaya za Kiswahili na uhalisia wake katika jamii. Kazi nyingi zimechunguza wahusika katika riwaya zisizo za Kiswahili kwenye jamii nyingine za Kiafrika. Aidha, pamoja na wahakiki kuingiza kipengele cha wahusika katika kazi zao hakuna utafiti uliofanywa kulinganisha tabia za wahusika wa riwaya mmoja na nyingine. Jambo ambalo linatufanya tujiulize hivi tabia za wahusika wakuu zilizobainishwa na mwandishi mmoja zinafanana na kutofautianaje na zile zilizobainishwa na mwandishi mwingine.

Pia, wanachokiandika kwenye kazi zao kina uhalisia na hali ilivyo katika jamii au wanakengeuka uhalisia huo? Kutokana na hali hiyo, ni wazi kwamba utafiti unahitajika ili linganishi kati ya tabia za wahusika wakuu kutoka kazi za mwandishi mmoja na mwingine. Hili ndilo ombwe la kitaaluma ambalo mtafiti alikusudia kuliziba. Hivyo basi, katika kujaribu kuliziba ombwe hilo, utafiti huu umechunguza kulinganisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya ya Kiswahili ambapo riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano* zimeteuliwa kama sampuli ya riwaya za Kiswahili.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kazi tangulizi mbalinbali kuhusu tafiti na riwaya ambazo zinaelezea wahusika. Sura imeanza kwa kuelezea historia fupi ya riwaya ya

Kiswahili. Pia, sura hii imeendelea kuelezea dhana ya wahusika na tahakiki za riwaya za Kiswahili, tafiti kuhusu wahusika, kiunzi cha nadharia, pengo la utafiti na hitimisho la sura.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inajadili mikabala, mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kukusanya, kuzichambua, kuziwasilisha na kuzijadili data za utafiti huu. Jilala (2014) akimnukuu Spicer (2012) anasema utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana (taz. pia Creswel, 2009; Silverman, 2010). Kwa ujumla, sura hii inajadili eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, utafiti tangulizi, mbinu za ukusanyaji data, na hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika mji wa Zanzibar. Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani na uwandani ambapo ulifanyika katika maktaba mbalimbali za Zanzibar na Dar es Salaam ikiwemo maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (East African), maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), maktaba Kuu ya Zanzibar, maktaba ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) na maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kwamba utafiti huu ulilenga kupata na kusoma maandiko mbalimbali yaliyohusiana na utafiti, hivyo katika maktaba hizo ndiko kulikopatikana machapisho mbalimbali ambayo yalitupatia data za msingi za utafiti huu. Katika maktaba hizo.

### 3.2.1 Mbinu ya Mapitio ya Maandiko

Jilala (2014) anasema mbinu hii huhusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa

ya maandishi au mazungumzo. Mbinu hii iliambatana na usomaji na uchambuzi wa riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano*. Vilevile, mbinu hii ilihusisha usomaji, uchambuzi na uchunganuzi wa data katika vitabu na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti huu, kama vipeperushi, na taarifa za kwenye mtandao.

Hivyo mtafiti aliweza kupitia maandiko na kukusanya data za msingi kutoka katika riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano.* Mtafiti alipata data za mbinu ya uchambuzi wa tabia za wahusika kwa kusoma riwaya zote mbili kwa umakini mkubwa, ili kujua vipengele anavyopaswa kuvizingatia kwa umakini wakati wa usomaji wake. Alinukuu data hizo katika shajara kwa ajili ya uchambuzi kulingana na maswali ya utafiti ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

Aidha, data nyingine za utafiti huu zilipatikana kwa mtafiti kupitia maandiko yanayohusiana na utafiti huu, kutoka katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, maktaba ya East Africana ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, maktaba kuu ya Zanzibar na maktaba ya Baraza la Kiswahili la Zanzibar, pia katika tovuti mbalimbali. Kwa ujumla mbinu hii ilitusaidia kupata data za kutosha kuhusu tabia za wahusika ili kukamilisha malengo ya utafiti huu.

## 3.3 Zana za Utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia zana mbalimbali kama zifuatazo hapa chini:

### 3.3.1 Shajara

Kwa mujibu wa TUKI (2013), shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika utafiti

huu. Kwa kutumia zana hii, mtafiti aliandika katika shajara taarifa mbalimbali zilizotokana wakati wa utafiti.

### 3.3.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana ambayo mtafiti aliitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake.Komyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (BAKIZA, 2010). Mtafiti aliitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yahusuyo utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

### 3.3.3 Simu ya Mkononi

Simu ni chombo kinachopokea na kupeleka taarifa sehemu mbalimbali kutokana na mitambo yake ilivyosukwa kitaalamu. Pia simu hutumika kurekodi mazungumzo, kuandika ujumbe, kupiga picha na kufanya kazi nyingine mbalimbali hata za mahesabu. Katika utafiti huu, simu ilitumika kuwasiana na watafitiwa ili kuweka miadi ya muda wa kukutana.

### 3.3.4 Vifaa vya Kunukulia

Karatasi, kalamu na wino wa kufutia, mtafiti alitumia vifaa hivi katika kuandikia maelezo mbali mbali muhimu aliyoyapata kutoka kwa watafitiwa wake, aidha alitumia vifaa hivyo kunukulia na kuchukua dondoo kutoka katika maandiko mengine tofauti ambayo atayapitia

## 3.4 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali

ya utafiti husika. Wakiunga mkono hoja hii Bogdan na Biklen (1992), wakinukuliwa na Omari (2011), wanaeleza kuwa, hii ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti husika. Zipo mbinu mbalimbali za uchambuzi wa data lakini data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya Uchambuzi maudhui.

Kombo na Tromp (2006), wanaeleza kuwa mbinu ya uchambuzi maudhui ni mbinu ambayo huziweka mada kulingana na jinsi zinavyofanana na kuhusiana. Dhana kuu au dhamira kuu hubainishwa na kuwekwa pamoja. Utafiti huu uliitumia mbinu hii kuzisoma riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* kwa lengo la kupata uelewa na kubainisha tabia za wahusika katika riwaya hizo. Sababu ya kuitumia mbinu hii ni kwamba, mbinu hii ni mbinu ambayo imekuwa ikitumiwa na watafiti wengi wa kazi za fasihi.

Wakati wa kukusanya data za utafiti huu, mtafiti aliandaa daftari au shajara maalum kwa ajili ya kudondoa data za utafiti kwa kusoma maandiko na kubaini tabia za wahusika. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi maudhui, mtafiti aliweka na kuzipanga katika kundi moja data zilizofanana na kuhusiana. Kwa kufanya hivi, ilisaidia kuchambua na kujadili data za utafiti kulingana na malengo mahususi na maswali ya utafiti. Vile vile ilisaidia kurahisisha zoezi la ulinganisha na kutafautisha. Mbinu hii ilionekana kufaa zaidi katika kuchambua data za utafiti na kurahisisha uelewekaji wake kwa msomaji kwani iliwezesha kuzipanga na kuzilinganisha na kuzilinganua data hizo na hivyo kuleta maana kwa data hizo ili kuwezesha mawazo ya jumla kubainika kulingana na malengo ya utafiti. Vilevile, utafiti huu umetumia majedwali katika kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti huu.

## 3.5 Uzingatifu wa Maadili ya Utafiti

Kwa mujibu wa Padgett (2002), katika utafiti wowote masuala ya maadili hujitokeza na yanapaswa kuzingatiwa katika aina zote za utafiti. Maadili hayo ni pamoja na kuomba ridhaa na kibali cha ruhusa ya kufanya utafiti katika eneo la utafiti, usiri, uwazi, ushiriki wa hiari kwa wahojiwa, utiifu na uvumilivu.

Kwa hivyo, sehemu hii inabainisha maadili ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia katika mchakato mzima wa utafiti wake kuanzia wakati wa ukusanyaji wa data ya utafiti na baada ya uchambuzi wa data. Kwa vile, utafiti huu ulihusisha watu kutoka maeneo mbalimbali na mtafiti kutembelea taasisi mbalimbali za kiserikali na kibinafsi, na kila sehemu ina taratibu zake hivyo mtafiti alipaswa kuzingatia maadili ya utafiti.

Kutokana na sababu hizi, mtafiti kabla ya kuanza kufanya utafiti alitafuta kibali cha kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kibali ambacho kilimwezesha kupewa kibali kutoka mamlaka inayohusika na utoaji wa vibali vya utafiti kwa upande wa Zanzibar. Kibali kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Zanzibar kilimsaidia mtafiti kuingia katika maeneo ya utafiti wake na kumlinda kisheria. Wakati akiwa maeneo yanayohusika mtafiti kabla ya kuwaona watafitiwa aliwaona viongozi wenye mamlaka katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mtafiti alifika kwa masheha wa shehiya ili kujitambulisha kwa kuonesha kibali cha utafiti ili kuwatoa wasiwasi kuhusu uwepo wake na shughuli iliyomsukuma kuwepo hapo.

Pia, baada ya kupata kibali cha kuanza kazi ya utafiti mtafiti aliomba ridhaa kwa washiriki wake bila ya kuwalazimisha na wale waliokataa kushiriki aliwaachia. Pia, watu hao aliwaridhia kwa upole bila ya kuwalazimisha, kwa sababu Kombo na

Tromp (2006), wanaeleza kuwa ni muhimu sana washiriki wa utafiti wakashiriki kwa kujitolea bila kulazimishwa. Hivyo basi washiriki wote waliotoa data walifanya hivyo kwa hiari yao. Mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti wake, kuanzia lengo kuu na kwa nini anahitaji data hizo mpaka matarajio yake, ili kupata maoni ya watafitiwa. Baada ya kutoa lengo la utafiti wahojiwa waliuliza maswali ya kutaka ufafanuzi juu tabia za wahusika.

Hivyo, mtafiti alitoa maalezo ya kina na watafitiwa wakaridhika juu ya hilo, hii ilisaidia kurahisisha zoezi zima la utafiti ambapo wahojiwa walioshiriki katika kutoa data za utafiti huu, walitoa data hizo kwa hiari na kwa uamuzi wao bila kutumia nguvu na mtafiti. Wakati wa kukusanya taarifa mtafiti aliuliza maswali yake kwa usahihi na kwa sauti ili kufahamika kwa urahisi na kuweka kumbukumbu za taarifa zote katika sehemu inayohusika.

Mtafiti pia, alizingatia suala la usiri kwa kuwaahidi na kuwahakikishia washiriki waliotoa taarifa za utafiti huu kuwa data walizozitoa zitakuwa ni siri ya mtafiti na mhojiwa na kutumika kwa ajili ya malengo ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Kwa kufanya hivyo, wahojiwa hawakutakiwa kutaja majina yao wakati wa kutoa taarifa ili kulinda siri ya mtoa data. Kwa kulinda ahadi hii ya usiri mtafiti aliyoitoa kwa wahojiwa wake, matokeo yote ya utafiti huu hakuna urejelezi wa jina la mtoa taarifa lilitoandikwa katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Kama wanavyoeleza Kombo na Tromp (2006) kwamba, washiriki hawanabudi kuhakikishiwa na watafiti kuwa usiri wa data wanazozitoa utazingatiwa. Hii ni pamoja na kuwahakikishia kuwa, data hizo hazitatumika vinginevyo zaidi ya kutimiza malengo ya utafiti huu na bila kubainisha chanzo cha data hizo.

Kwa mantiki hiyo, suala la faragha lilizingatiwa wakati wa ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa. Kwa sababu mtafiti alitambua kuwa kila mshiriki ana haki ya kupata faragha. Watafitiwa wengine walitaka usaili ufanyike majumbani kwao hasa wazee, mtafiti aliamua kuwafuata huko majumbani kwao kwa ajili ya kupata ufaragha na kupata data za uhakika kwani mtafiti alipofuata matakwa ya mtafitiwa aliweza kujisikia kuwa yuko huru na kutoa data za uhakika.

Pia, sayansi ya utafiti umezingatiwa na kufuatwa kabla ya kukusanya data, wakati wa ukusanyaji wa data, baada ya ukusanyaji wa data na katika uchambuzi wa data. Mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu zimezingatia misingi ya kufanya uchunguzi wa sayansi jamii.

## 3.6 Hitimisho

Sura hii imejadili mbinu za utafiti ambapo imeanza kujadili eneo la utafiti lilikuwa ni Zanzibar. Wakati walengwa wa utafiti huu ni wasanii na watunzi wa riwaya lengwa za utafiti huu na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili (riwaya) wa Chuo Kikuu cha SUZA. Mbinu za usampulishaji zilizotumika ni mbili yaani; mbinu ya uteuzi ya usampulishaji huru na mbinu ya uteuzi rahisi. Sura hii pia imebainisha na kujadili mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ambazo ni; mbinu ya mapitio ya machapisho, dodoso na uwandani. Baada ya kujadili mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sura inayofuata inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti huu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data iliyokusanywa kwa ajili ya kukamisha malengo ya utafiti huu. Sura inaanza kwa kutoa muhutasari wa riwaya teule, kubainisha na kujadili tabia za wahusika wakuu wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* na kulinganisha tabia za wahusika waliobainishwa katika riwaya hizo. Kwa hiyo, data iliyokusanywa imewasilishwa ili kujibu maswali ya utafiti huu, data hiyo imechambuliwa kwa mkabala usio wa kiidadi na kufafanuliwa kwa mbinu ya maelezo.

## 4.2 Muhutasari wa Riwaya ya Teule

Katika sehemu hii tunajadili lengo mahususi la kwanza ambalo lilikuwa linataka kutoa muhutasari wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* ambazo ziliteuliwa na kuchambuliwa katika utafiti huu. Lakini kabla hatujaanza kulifafanua lengo la kwanza itakuwa vyema tukaeleza kwamba uchambuzi wa tabia za wahusika wakuu katika riwaya hizi umezingatia dhamira ambazo zimejengwa na tabia za wahusika katika riwaya za Kiswahili ambazo zinaakisi maisha ya jamii. Sasa tuanze kuchunguza muhutasari wa riwaya teule ambapo tutaanza na Kusadikika na kumalizia riwaya ya utengano.

### 4.2.1 Muhutasari wa Riwaya ya *Kusadikika*

*Kusadikika* ni riwaya ya Shaaban Robert iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1951 na *Thomas Nelson and Sons Limited*. Hii ni moja kati ya riwaya

maarufu za Shaaban Robert. Ni riwaya iliyojaa ufundi wa lugha na usanifu komavu. Riwaya hii imebeba ujumbe mzito unaoakisi moja kwa moja jamii za Kiafrika. Riwaya ya *Kusadikika* inaelezea nchi ya Kusadikika ambayo mwandishi ameanza kwa kusimulia tukio la kushitakiwa kwa mhusika Karama ambaye ni mhusika mkuu wa riwaya hii kwa tuhuma kwamba alitaka kuihujumu serikali ya Kusadikika.

Mhusika Majivuno ambaye alikuwa Waziri mkuu wa nchi ya Kusadikika aliwasilisha mashitaka mbele ya mahakama kwamba Karama alikuwa akitoa elimu ya sheria, jambo ambalo kwa mtazamo wa Waziri Majivuno lingewafanya raia wa Kusadikika kuelewa haki zao. Hali ambayo ingesababisha wananchi kutotii serikali au wangezuia unyanyasasaji, ukandamizaji, uonevu na uongozi mbaya ulioendeshwa na watawala wa Kusadikika. Hivyo, waziri Majivuno alipata hofu kubwa sana akidhani kwamba jambo hilo likiachwa likiendelea basi serikali ya Kusadikika itafikia ukomo hapo.

Riwaya inaendelea kusimulia jinsi mshitakiwa Karama alivyowasilisha utetezi wake mbele ya mahakama ya Kusadikika ambayo iliundwa na mfalme na madiwani wa Kusadikika. Mhusika Karama aliwasilisha utetezi wake kutoa uthibitisho wa namna serikali ya Kusadikika ilivyoshindwa kuthamini michango ya wananchi wake. Karama alianza kuelezea historia ya wajumbe mbalimbali waliojitolea kwa gharama zao kwenda nchi za mbali kufanya utafiti wa jinsi ya kuleta maendeleo katika nchi yao.

Masimulizi ya Karama yaliwabainisha wajumbe sita ambao walitumwa kwenye nchi sita ambazo zimepakana na nchi ya Kusadikika. Nchi hizo ni kama vile nchi ya upande wa Kaskazini, Mashariki, Kusini, Magharibi, Mbinguni na Ardhini. Mwisho

wake wajumbe hao ambao walikuwa wazalendo kwa nchi yao walifungwa jela mara tu waliporejea kutoka kwenye nchi walizotumwa. Mwandishi wa riwaya hii anahitimisha kwa kuelezea hukumu ya Karama ambapo mahakama iliyosimamiwa na mfalme na madiwani ilivyomwachia huru mshitakiwa kwa sababu hakuwa na hatia. Hatimaye, mfalme akaamuru wajumbe wote sita waliokuwa wanatumikia kifungo waache huru na kulipwa fidia kutokana na udhalilishaji walioanyiwa wakati wao walijitolea kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yao.

### 4.2.2 Muhutasari wa Riwaya ya Utengano

*Utengano* ni riwaya iliyotungwa na mwandishi Said Ahmed Mohamed mwanzoni mwa miaka ya 1980 mambo mengi sana. Riwaya ya Utengano inajikita juu ya familia ya Makusudi. Riwaya hii inazungumzia kuvunjika kwa aila hiyo pamoja na misukosuko inayoikumba aila hiyo. Hivyo, kutokana na kuvunjika huko kwa mujibu wa kisa cha hadithi ni tabia ya bwana Makusudi na jinsi tabia hiyo inavyomuathiri mkewe na watoto wake pamoja na umma kwa jumla. Bwana Makusudi alikuwa ni mtu na familia yake, mke wake aliyeitwa Tamima na watoto wawili mmoja wa kike na mmoja wa kiume. Makusudi alionekana kuwa Mcha mungu akisomesha darsa kama alivyodai mwenyewe. Alikuwa mwanzilishi wa chama Mwafrika kilichopigania uhuru wa Mwafrika kutoka kwa wakoloni wa Kiarabu na Kiingereza. Baada ya kupatikana uhuru aliwekwa mkuu wa wilaya na pia akawa Mkurugenzi wa Bima ya Taifa.

Pamoja na kutaka kuonekana mcha mungu Makusudi alikuwa mfedhuli. Makusudi alikua mume mzinifu alishiriki hafiriti, mchafu huku akijivika guo la ucha mungu

yaani kila jumamosi ya wiki ya mwisho alimtembelea Kazija kama mwanamke wake.

Bi Kazija baada ya chuki aliyokuwa nayo juu ya bwana Makusudi kuona namna anavyowalaghai wanawake aliamua kuwagonganisha vichwa baina ya Makusudi na mwanawe Mussa, na bwana Makusudi aliamua kutaka kumuua mwanawe kwa kuona anatembea na mwanamke wake Kazija.

Maimuna aliamua kukimbia nyumbani kwao kwa kutoroshwa na Bi Farashuu na Bi Tamima aliburuzwa sana na bwana Makusudi akiona kuwa yeye anahusika. Na Mussa naye aliamua kutoroka kwao na asijulikane wapi ameelekea na Bi Tamima naye alipewa talaka na bwana makusudi. Baada ya Maimuna kuondoka nyumbani, kwa mawazo ya kutaka kupata uhuru wake wakutenda atakalo, alikuja kushtukia ametumbukia katika maisha machafu ya zinaa. Alikuwa muuzaji wa pombe na muimbaji, baada ya Maimuna urembo na ujana kumkauka aliamua kuolewa na kijana aitwae Kabi mjukuu wa Bi Farashuu.

Bwana Makusudi alifungwa jela kutokana na maovu aliyoaakiyatenda baadaye alitolewa jela na alikaa kwa miaka miwili alirejea nyumbani asiwe na mtu wa kumhurumia wala watumishi wa kumhudumia. Makusudi aliyakosa mapenzi ya mkewe na watoto wake alifanikiwa kumpata mtoto wake Mussa katika jitihada za kumtafuta Maimuna na Bi Tamima mkewe. Makusudi hakufanikiwa kumpata Maimuna na kumrejesha nyumbani, Maimuna kama mama yake hakukubali msamaha wa baba yake wala hakuwa tayari kumsamehe. Ugonjwa na upweke aliokuwa nao Makusudi baada ya kutoka kifungoni ulimfanya ayajutie matendo

yake. Hadi mwisho wa riwaya hii ni dhahiri kuwa kuna Utengano ijapokuwa kila mmoja anamsamehe aliemkosea hakuna ishara ya kuondoka kwa utengano.

### 4.3 Kubainisha na Kujadili Tabia za Wahusika

Ubainishaji wa tabia za wahusika umefanywa kwa kufuata hatua kuu mbili. Hatua ya kwanza mtafiti amesoma riwaya alizoziteua. Hatua hii imeenda sambamba na hatua ya pili ambayo ilikuwa ni kunukuu mazungumzo yanayowahusu wahusika. Mazungumzo hayo yamemsaidia mtafiti kujua tabia za wahusika aliowatafiti. Uchambuzi wa tabia umefanyika kwa kuzingatia mtunzi anasema nini kumuhusu mhusika fulani, wahusika wengine wanasema nini kuhusu mhusika huyo na yeye mwenyewe anasema nini kuhusu yeye mwenyewe.

Tunawaangalia wahusika wakuu wa riwaya ya *Utengano* tunamkuta Bwana Makusudi ambae aliitawala riwaya yote nzima mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Pia tunamuona Maimuna ambaye alikuwa ni kielelezo cha kutosha kati ya wahusika, miongoni mwa wahusika wakuu ni Kazija ambaye alikuwa na jitihada ya kutaka kuepukana na vitimbwi vya watu waovu. Farashuu pia ni miongoni mwa wahusika wakuu wa riwaya ya Utengano.

#### 4.3.1 Tabia za Wahusika Wakuu wa Kusadikika

*Kusadikika* ina wahusika wa aina mbili. Aina ya kwanza ni wahusika wanaojulikana kuwa washiriki. Wahusika wa aina hii ni wale walioshiriki kwa namna fulani katika hadithi. Wahusika hawa ni kama vile Karama, Majivuno, Mfalme, Madiwani, Taadabuni, Komeni, Fujo, Boramimi na kadhalika. Kundi la pili ni la wale wahusika aliowatumia Karama katika kufikia lengo lake. Wahusika hawa hawatokei kimwili,

wanatokea kimawazo tu. Kundi hili lina wahusika: Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini.

Katika makundi haya, wako pia wahusika wakuu na wabusika wasaidizi. Kwa upande mwingine, ujenzi wa wahusika hawa ni wa aina mbili: Kuna wale wahusika ambao wamejengwa na tabia zao. Kwa mfano, Majivuno alikuwa na majivuno, Karama alikuwa mwenye karama kubwa, Fadhili alikuwa na fadhila na kadhalika. Aidha, kuna pia kuwajenga wahusika hawa wanavyoonekana. Kwa mfano, tunaambiwa: "Kwa wasifu wa nje, mshtakiwa Karama alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu..." (uk. 8). Pengine tungewaangalia wahusika hawa mmoja mmoja.

**4.3.1.1 Karama**

Huyu ni mhusika mkuu wa *Kusadikika.* Karama ni raia aliyeshtakiwa na Waziri Majivuno kwa kosa la kupinga Sheria za nchi ya Kusadikika. Kwa upande wa baadhi ya watu wenye mamlaka, Karama alidhaniwa kuwa anagombea cheo au madaraka. Aidha alihesabiwa kuwa ni mkosefu wa utii; na mtovu wa shukrani. Karama alishukiwa pia kuwa na wafuasi wengi waliokuwa wakimuunga mkono; katika taaluma ya elimu ya kufundisha sheria.

Karama alikuwa mshtakiwa wa kwanza katika historia ya Kusadikika kuruhusiwa kujitetea. Ni mtu wa kwanza nchini Kusadikika aliyeweza kubadili sheria za nchi yake, Ni shujaa aliyeweza kupambana na kuwaokoa wenzake waliokuwa kwenye kifungo cha maisha.

Katika wasifu wake wa ndani na nje, Karama alikuwa na sifa zifuatazo, kimaumbile, umbo lake lilikuwa baya. Alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu. Kwa wasifu wa ndani Karama alikuwa na ajabu tatu: ubongo wa hekima kichwani, moyo wa ujasiri kifuani na kinywani ulimi wa ufasaha. Ni mkweli na jasiri. Hivi ni vipawa vilivyounda siri kubwa katika maisha ya Karama. Alikuwa na tabia ya kuficha siri kama kaburi lifunikavyo maiti. Karama ni jina linalosadifu kauli na matendo yake. Karama ni mfano wa kuigwa.

#### 4.3.1.2 Majivuno

Majivuno ni Waziri Mkuu wa Kusadikika. Mwandishi anamjenga kikejeli kuwa alikuwa mtu mwenye haiba (upendo) na uhodari mwingi, jambo ambalo halikuwa sahihi. Alikuwa na majivuno. Alitawala kwa muda mrefu, akiwa waziri katika nyakati mbalimbali za wafalme watatu. AIikuwa mtu mwenye inda na tadi, Majivuno alimshtaki Karama kuwa alikuwa akipingana na sheria za Kusadikika, Alikuwa mtu mwenye chuki na wivu mbaya. Majivuno ndiye aliyekuwa msemaji mkuu katika kesi iliyomhusu Karama. Alikuwa mtu mwenye dharau kubwa, na alijihesabu kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya Wasadiki wote ikiwe kwa pamoja. Alitumia nafasi na cheo chake kupotosha ukweli, kama vile alipotoa fasiri kuwa, "Uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria". Majivuno si mfano bora wa kuigwa.

#### 4.3.1.3 Wajumbe Sita

Hawa ni wahusika sita ambao walitumiwa na Karama katika kujitetea. Kwanza, kuna mjumbe wa Kaskazini aliyejulikana kwa jina la Buruhani. Kazi ya Buruhani ilikuwa

kusafiri, kutalii na kuandika habari za mambo ya nchi za kigeni aliyoyaona kwamba yangestawisha Kusadikika. Karama anaelezea mkasa wa Buruhani kuwa baada ya kukusanya na kuleta aliyoyaona yanafaa, aliaibishwa na kudaiwa ameleta uzushi usio na faida katika nchi ya Kusadikika. Alitumbukizwa kifungoni: Kifungo cha maisha.

Fadhili ni mjumbe wa pili aliyetumwa Mashariki. Alisafiri kuelekea Mashariki na aliporudi alileta ujumbe kuwa wakazi wa nchi za Mashariki waliuchukia uchokozi, na waliuona kama kitu kikubwa cha aibu: Watu hawa pia waliviapiza vita ama laana ipitayo kiasi kwa viumbe waliojaliwa busara ya haki; moyo wa wema; ulimi na ufasaha na nasaha; masikio ya kusikilizana, macho ya uongozi; pua ya kutambua harufu; ushirika wa amani; ajali moja na Mungu mmoja. Badala ya kushangiliwa, aliitwa mwongo, mwoga na mwotaji wa ndoto zisizotabirika. Alidharauliwa na kudhalilishwa.

Mjumbe wa Kusini alikuwa na jukumu la kuona mambo yalivyo katika nchi tatu za Juju, Hasira na Kiasi. Mjumbe huyu aliitwa Kabuli. Alipatwa na matatizo mengi, na aliporudi alileta ujumbe juu ya matumizi bora ya mamlaka, kutunza heshima za watu, kutotenda maovu, kutotumia nguvu kusuluhusha matatizo, n.k. Lakini roalipo ya Kabuli yalikuwa ni adhabu kali ya kifungo cha maisha.

Auni alikuwa mjumbe aliyekwenda Magharibi. Auni aliona watu walipendana wakaishi bila chuki; bughudha, na kuheshimiana. Aliwaona watu walioheshimu ndoa wakazaa watoto na kuwalea. Alipoleta ushauri huo Kusadikika, alipatilizwa adhabu kali ya kitungo na kazi ngumu.

Ridhaa alitumwa Mbinguni. Aliona hali ya ujenzi bora, mabustani, uchoraji, watu walitunza siri, nafasi ya kubadilishwa viongozi kwa kuzingatia utaratibu maalumu na mengineyo. Lakini kama ilivyokuwa kwa wengine Ridhaa naye aliadhibiwa kwa upanga uleule, kifungo cha maisha.

Mjumbe wa mwisho alikuwa aliyekwenda Ardhi aliitwa Amini. Yeye safari zake zilikuwa kupitia ndege Mangara aliyekuwa akila duniani na kulala nyumbani. Ujumbe wa Amini nchini Kusadikika ni kwamba watu wa Ardhi walikuwa waadilifu na walipaswa kuigwa. Lakini alionekana hakufanya jambo la maana, alihukumiwa kifungo cha maisha.

Kwa kutumia wahusika hawa, Karama amejijengea uhalali wa thamani ya utetezi wake. Falsafa inayojitokeza ni kuwa Karama ni sawa na wajumbe sita waliokwenda sehemu mbalimbali ili kuleta "elimu" kwa Wasadikika, hawakuthaminiwa kama Majivuno asivyomthamini Karama. Huruma iliyojengwa juu ya wajumbe hawa ndiyo iliyomwokoa Karama.

### 4.3.2 Tabia za Wahusika Wakuu wa Utengano

Katika sehemu hii tumeeleza tabia za wahusika wakuu wa riwaya ya *Utengano*. Wahusika ambao tumewabainisha na kuwajadili ni Makusudi, Maimuna, Farashuu, Kazija na Mussa.

#### 4.3.2.1 Makusudi

Makusudi ni muhusika mkuu wa riwaya ya *Utengano*, yeye anashika nafasi kubwa katika riwaya hii. Tunapomkuta Bwana Makusudi kwa mara ya kwanza (uk:11-12)

tunakutana na mwanamume mdanganyifu. Mwanamume ambaye haheshimu miko ya ndoa, anatoka nje kuwafuata wanawake wengine. Makusudi ni kiongozi asiyehishimu madaraka yake ni mwingi wa hadaa na udanganyifu. Makusudi alikuwa mtu dhalmu, afiriti na mwingi wa maovu. Makusudi anajielewa kuwa afanyayo siyo na ni kinyume na maadili ya jamii. Anajali sana nafsi yake, Anajali ile nafsi ya kujitajirisha mwenyewe. (uk:12) Imani ya Makusudi juu ya wanawake ni jambo litishalo.kwake mwanamke si kitu (uk:15) Imani hii ndio iliyomfanya kumtesa Mwanasururu. Kuwatawisha Maimuna na Tamima (uk:19) anawabeza na kuwadharau wanawake mathalan Bint Kocho (uk:51) Mwandishi anatuambia kwamba Makusudi alitokana na tabaka la wachochole "tabaka la wakulima na wafanyakazi yaani tabaka la wanyonge" (uk: 17) alikuwa mmoja wa waanzilishi wa chama cha Mwafrika kilichodai uhuru wa Mwafrika na kumuondoa mkoloni.

Alikuwa kiongozi shupavu mwenye nia thabiti. Alipigania uhuru wananchi yake nia moja. Licha ya yote hayo makusudi alikuwa mwalimu wa dini. Uhuru ulipopatikana Makusudi alipewa madaraka kama mkuu wa wilaya. Baada ya kuyapata madaraka aliisaliti ile nia thabiti ya kutetea wananchi. Aakapata nafasi ya kunyanganya wananchi. Katika wale wengi aliowadhulumu kuwahini na kuwafanya watumwa walikuwa wanawake (uk: 43). Matendo yake maovu yalimpeleka jela.

**4.3.2.2 Maimuna**

Tunapokutana na Maimuna tunakutana na mwanamke mtawa. Anatawishwa na kuekwa ndani na baba yake Bwana Makusudi kutawishwa huku kuna mnyima haki na uhuru Maimuna. Maimuna ni muhusika anayeonewa na anaefungiwa ndani kutumika kiutumwa. Kufungiwa huku kuna mfanya maimuna kuwa mtoro (uk:19).

Utoro wake una nia njema, yaani anataka kujinyakulia uhuru wake, apate kuishi akiwa uuru na awe na hadhi ya kiutu. Maimuna ni mtiifu kwa sababu yenyewe ni kwamba muda mrefu wa utawa, Maimuna yu radhi kusononeka na kuumia badala ya kuivunja miko ya baba yake.

Maimuna si mjinga anaufahamu udhalimu wa baba yake. Maonevu wayapatayo wanawake na mnyanyaso wa wanaume dhidi ya wanawake. (uk:20,23) Maimuna katika utumwa wake hakupata kutoka nje pasi na ruhusa ya baba yake na kufungiwa huku kulimwathiri sana Maimuna na kumfanya boza. Mara nyingi alilia na kuona kama ametengwa na jamii. Maimuna aliamua kujitafutia uhuru wake na akaamua kutoka nje na kuangukia kwenye balaa la zinaa. Haya yalimfanya kila siku kujikinga na hujuma za wanaume waovu (uk:56-57). Maimuna hakuzoea fujo wala zogo (uk:63). Shida alizopata Maimuna zilimfanya awe jasiri na kumwerevusha na mambo ya dunia.

**4.3.2.3 Kazija**

Kazija ni muhusika tunaekutana nae katika riwaya ya utengano. Ni muhusika mwenye chuki na kisasi kwa wanaume. Kazija anafahamu kwamba mwanamke daima yumo katika utumwa wa kulazimishwa. Utumwa ambao umemdhalilisha mwanamke na kumwacha kiumbe dhaifu kisichokua na maisha (uk:1) Kazija ni mwanamke aliepevuka kikweli katika kuidai haki yake pamoja na maslahi ya wanawake. Hana kificho katika kuwaambia wanaume udhalimu wao. Kazija ni muhusika wa kike wa kwanza anaetambua kuwa mwanamke anayenyimwa uhuru ili awe rahisi kutawaliwa (uk:7). Kazija lijifunza kupigania na kudai haki yake kwa ujasiri. Kazija ni mtambuzi wa udanganyifu, kiburi na unafiki wa viongozi. Kazija si

mjinga hapo alipo na baada ya kuutambua unafiki wa viongozi anujua wajibu wake katika kuutilia kikomo unafiki huo. Anaudhihirisha unafiki wa Makusudi na Zanga (uk.80-82). Huyu ni mwanamke anayefahamu nafasi yake katika jumuia yake. Kupitia muhusika huyu mwandishi anatwambia si wanawake wote wasiotambua wajibu wao wanawake kama Kazija ndio wanaotegemewa katika vita vya ukombozi wa wanawake. Labda pia mwandishi anasema wanawake kama hawa ni nadra sana kupatikana. Jambo linalomtambulisha kazija niule ujasiri wake katika kukataa madhila na kuikabili dunia kama mtu akitakacho.

#### 4.3.2.4 Farashuu

Farashuu ni mkunga wa kienyeji anayeishi katika mtaa wa Madongo Mporomoko mtaa wa wanapoishi wachochole na makabwela. Farashuu ni myonge anayetokana na tabaka la chini. Anaishi kwa kuuza vitumbua na wakati mwingine huitwa kwa kufanya ukunga. Zamani alikuwa mkwewe Bwana Makusudi ambaye alimtesa bintiye Farashuu-Mwanasururu na kusababisha kifo chake. Kifo cha Mwanasururu kilichochea kisasi moyoni mwa Farashuu tunamuona ni mwanamke mwenye kisasi kwa Makusudi. Ni mwanamke mpole na mtulivu mwenye kisasi kwa yeyote amtendaye maovu.

Hataki kufanya kazi yeyote ya ujeuri; jambo ambalo limekuza imani fulani katika mawazo yake kwamba (uk. 31). Labda umuhimu mkubwa wa Farashuu katika riwaya hii mbali na kuwakilisha wanyonge. Yeye ndie chanzo cha utengano wa familia ya Makusudi. Farashuu ndiye aliemtia maneno binti Kocho na kumtoa nyumbani kwao na kumtenga na wazazi wake. (uk. 31). Kuharibika kwa Maimuna

kunaweza kuhusishwa na farashuu moja kwa moja. Talaka ya Tamima nayo inaweza kuhusishwa na Farashuu moja kwa moja. Na kuharibika kwa Maimuna kunahusishwa na mkabala huohuo. Alishirikiana na Kazija kumwandalia fumanizi Makusudi na mwanawe Mussa. Yeye ndiye aliyemtosa Maimuna katika zinaa. (uk. 169). Jambo ambalo linatukumbusha umuhimu wa Farashuu ni kisasi. Visasi vilivyo katika riwaya hii ambapo tukichunguza sana vinahusiana na muhusika huyu.

#### 4.3.2.5 Mussa

Mussa ni mtoto wa kiume wa Bwana Makusudi ambaye akiwa katika umri mdogo Mussa ananza kuiga mambo mabaya ya baba yake Makusudi. Mambo yenyewe ni kama uafiriti na ukware wake unaonekana pale anapomwandama Kazija. Kazija ni mtu mzima rika labda la mama yake Mussa. Lakini Mussa haoni taabu kumwandama. Mussa ni mlevi anayachapa maji kikweli kweli. Tena katika kufanana na baba yake anaiga hata mawazo yake yaani hata yeye anawadharau wanawake (uk. 7). Mwandishi pia, amemnyima nafasi ya kukua.Baada lile fumanizi na baba yake. Mussa anatoweka bila kujulikana alipotelea wapi. Baada ya kifungo cha baba yake Mussa alikuwa yuko mwaka wa tatu chuo kikuu, amekuwa msomi, tena daktari aliamua kuyaacha machafu yote aliyokuwa nayo. Makusudi alipokuwa anamtafuta Maimuna anakutana na Mussa. Makusudi pindi alipopata maradhi anatibiwa na Mussa na anaamua kutoa damu na kumsaidia baba yake, damu hii inaondoa uhasama uliopo wa Mussa na baba yake. Mussa anageuka mtu mwenye imani na kumhurumia Maimuna mdogo wake pamoja na Tamima mama yake. Mussa anaungana na baba yake kuukata utengano uliopo na aila yao Mussa ni muhusika asiyefahamika kwa urahisi.

Mwandishi Said Ahmed, hivi ndivyo alivyowatayarisha na kuwaumba wahusika wake kwa tabia hizo zilizoelezwa hapo juu. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia tunaona kua Muandishi Said A Ahmed na Shaaban Robert wamefanikiwa kuwachora wahusika wao katika uhalisia wajammi husika. Hivyo basi ni dhahiri kwamba nadharia hii ya uhalisia iliyotumiwa na waandishi hawa imeweza kusawiri mazingira halisi yaliokusudiwa na kupeleka ujumbe halisi wa waandishi hawa.

## 4.4 Kulinganisha na Kutafautisha Tabia za Wahusika

Katika sehemu hii tunajielekeza kujadili lengo letu la tatu ambalo lilitaka kulinganisha tabia za wahusika wa riwaya hizi. Wasanii wanapoandika kazi ya Sanaa huwaumba wahusika na kuwabebesha tabia tofauti, aidha tabia hizo huakisi jamii husika kazi hizo za kubuni au za uhalisia. Katika uumbaji wa tabia hizo,huwa kuna kulingana na kutofautiana baina ya wahusika wa kitabu kimoja na kingine. Katika kitabu cha kusadikika na kitabu cha utengano,wasanii wamejaribu kuakisi hoja kama ifuatavyo.

### 4.4.1 Makusudi na Majivuno

Msanii amewachukua wahusika hawa na kuwabebesha dhamira ya uongozi katika jamii yake. Ambapo amemchora Makusudi kama kiongozi katika jamii yake. Makusudi alikuwa mtetezi wa haki na kiongozi shupavu mpaka dakika ya mwisho, pia pia alikuwa muasisi wa chama cha waafrika. (uk. 17).

Majivuno alikuwa ni kiongozi wa serikali ya Kusadikika. (uk. 1) waziri wa Kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba na uhodari mwingi hivyo aliitwa majivuno. Makusudi mwanzo alitetea wanyonge na kuhakikisha haki na usawa unatendeka

katika jamii ijapokuwa mwishoni aliacha kazi hio na akaamua kuwa mtu mdhalimu na msalitina kujificha katika kichaka cha uchamungu na hasa kwa vile ni mtaalam kasoma dini sana  ni mcha mungu atakuwa na ngao kubwa ya kuficha utashi wake. (uk. 17).

Majivuno hakutokea kuwa mtetezi wa wanyonge bali alitokea katika Taifa la Kusadikika Taifa ambalo halikujali haki za raia utetezi katika sharia wala ustawi wa maendeleo katika jamii yake. (uk. 7) Sheria za wasadikika zilikuwa haziamuru mshtakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshtaki.Aidha mfanano mwingine wa tabia za wahusika hawa wawili ni tadi, inda na kiburi.

Makusudi alifanya tadi,inda na kiburi kea kuamini kuwa alikuwa na elimu sana ya dini na mtaalam wa kupigiwa mfano, hivyo ikamfanya aamini akafanya atakalo huku akijificha katika kichaka cha uchamungu. (uk. 17). Wakati majivuno kwa kuwa alihudumu kwa miaka mingi katika serikali ya kusadikika ndio iliyompa kibri na kujiona yeye ndie kila kitu. (uk. 4). Walakini kwa nia yangu njema na saburi ambayo kila waziri lazima kuwa nayo,mashtaka haya sikuyaleta barazani mpaka leo.

Makusudi pia alipenda sana masuala ya zinaa na pia alopenda kuwadhalilisha wanawakekatika jamii yake…"Mimi kweli si mwanamke, na wewekwako toka lini mwanamke akawa mtu.wangapi umewatenda, umemsahau farashuu na mwanawe." (uk. 15). Katika kudhihirisha tabia ya uzinifu bwana makusudi hakuwa mbali na Kazija kila mwisho wa wiki na hapo ushekhe na udini alikuwa akiuweka mbali. "Kazija alijitupa kwenya sofa ubavuni na kwa sauti nyororo,alianza leo nitakuvua

koti." (uk. 10-11). Aidha bwana Makusudi aliyapenda maswala haya na kuitelekeza familia yake.

Kwa upande wa Majivuno Msanii hakumchora na tabia ya anasa na uzinifu, hii ilisababishwa na msanii kutokuonesha nafasi ya mwanamke katika riwaya ya kusadikika kwa upana Zaidi.

### 4.4.2 Karama na Maimuna

Msanii amemchora Maimuna katika tabia tofauti.mfano, upole na mtiifu. Upole huu ndio uliompelekea mpaka kutawishwa na kuwa mtumwa wa hata fikra yake mwenyewe." Alivumbikwa ndani na baba yake na kwa kweli sasa ameshaiva,amenyimwa uhuru wa kutoka.Nae amemtii baba yake siku zote bila ya suali. (uk. 23).

Karama ni muhusika kati ya wahusika wakuu katika riwaya ya kusadikika moja kati ya tabia zake nyingi ni tabia ya upole na unyenyekevu. Msanii alionesha tabia hii katika riwaya ya kusadikika pale alipoeleza "Basi pale kizimbani alipokuwa amesimama wima aliinama kwa unyenyekevu mbele ya baraza,alipoinuka,alipinuka kwa sauti ya taratibu lakini imara aliyavuta masikio ya baraza nzima kumsikiliza kama imamu aliekuwa akihutubu juu ya membari ya msikiti mkubwa. (uk. 9).

Ama katika tofauti ya tabia za wahusika hawa ni suala la elimu.Tukianza na Maimuna msanii amemchora kuwa ni mwanamke aliekosa elimu na kutawishwa na baba yake pasi na kutoka hata nje, hili lilimfanya maimuna hata kutokujua mazingira na mazingara yaliomzunguka. (uk. 23). Kwa upande wa Karama, Msanii amemchora

karama huku akimbebesha tabia muhimu ya kuwa na elimu, Karama alikuwa ni miongoni mwa raia wachache waliokuwa na elimu ambayo ilikuwa ngeni katika mji wa Kusadikika. ”Kwa hivyo alikusudia kuwa mwanasheria wa kwanza wa Kusadikika. (uk. 9).

Katika tabia ya ujasiri ambapo msanii amewabebesha wahusika hawa katika riwaya zao, amemchora maimuna kukata shauri la kukimbia ili kujitafutia uhuru wake nje ya utawala wa baba yake.” Kwa maimuna nje ilikuwa pepo ingawa alikuwa na duku duku la uchungu wa mama yake pamoja na wio wa kuwa yeye leo amekuwa mtoro, hakuacha kuona raha ya msisimuo wa baridi ya majilio ya alfajiri. (uk. 24).

Karama kwa upande wa karama msanii amemchora karama kuwa ni kijana shujaa nashupavu katika mji wa kusadikika, aliweza kuhatarisha maisha yake kwa kutetea haki za wasadikika katika utawala wa sharia na pia kutetea maendeleo ya nchi yake katika nyanja za kiuchumi na kijamii. Ujasiri huu ulidhihirisha pale aliposimamishwa mbele ya baraza la mfalme kwa kukabili mashtaka yaliowasilishwa dhidi yake.” Msema kwelihukimbiwa na rafiki zake. Nikipatwa na ajali kama hio sitaona wivu juu ya watu wawezao kudumu siku zote.siwezi kuikana kweli kwa kuchelea upweke wa kitambo nikajinyima ushirika wa milele unaotazamiwa kutokea baada ya kushidwa kwa uongo. (uk. 9).

Kwa upande wa Maimuna, msanii hakumchora kama ni mtetezi wa wanyonge katika jamii yake ni wengi waliodhulumiwa na unyanyasaji uliotokana na wanaume. Uhuru alioutaka Maimuna ulikuwa ni kujitoa katika makucha ya baba yake na kuishi maisha huru (uk. 24).

Kwa upande wa Karama msanii, amemchora muhusika kuwa ni mtetezi si wa haki zake tu bali hata kwa haki za wasadikika wote. Karama alipoona utawala wa kusadikika unakwenda pasi na kufuata sharia, utetezi juu ya mashtaka yake juu ya baraza aliomba apewe siku sita juu ya utetezi huo ambapo siku sita hizo alizitumia kuelezea madhila na mashaka wanayoyapata wajumbe waliotumwa na serikali ya kusadikika kwenda kusoma nje ya nchi na kuja na ushauri utakaoleta faida na maendeleo katika nchi zao jaza zao walitumbukia katika vifungu vya maisha.” Nachelea kuwa sababu zilizoniongoza kufikiri kama nilivyofanya zitataka muda wa siku sita kueleza kwa muhtasari” (uk. 10).

### 4.4.3 Kazija na Buruhani

Buruhani ni miongoni mwa wahusika waliooneshwa katika riwaya ya kusadikika ambapo msanii amemchora katika tabia tofauti. Ujasiri ni tabia muhimu ambayo mwanadamu yoyote anatakiwa kuwa nayo katika kufikia malengo aliyokusudia. Ujasiri ni nyenzo ya mapambano katika jamii, ujasiri wa Burhani ulimfanya akabiliane kupambana na vikwazo vingi katika safari yake,hadi kuhitimishwa.” Alijitolea sadaka katika ujasiri ambao misiba yake ilikuwa katika mwangaza lakini faraja zake zilikuwa katika kiza kikuu (uk.13).

Kazija ni muhusika ambaye mwadishi amembebesha tabia ya ujasiri, ujasiri wa Kazija ulikuwa ni kupambana na aina zote za uonevu na ukandamizaji.ujasiri wake pia ulimfanya kudai haki yake pamoja na kuyatetea maslahi ya wanawake. Hana kificho katika kuwaambia wanaume udhalimu wao.” Kazija alitwogwa na uchungu wake wa kila siku, nani yeye? nani tena kama si mwanamke. Nayule pale ubavuni pake nani si mwanamme? mwanamume elimu bora kwa mwanamume… (uk. 7).

Ama kwa upande wa tofauti walizonazo wahusika hawa mwandishi anatueleza kuwa Kazija hakuwa mstahamilivu wala hakuwa mwenye subra ya kusubiria yale yote yaliomkuta kwa makusudi, bali aliendeleza chuki na kisasi kuanzia kwa makusudi mwenyewe mpaka kwa wanaume wote.” Kazija anayachukia ndiye anayachukia. Kwanza anamchukia mwanamme anamchukia kwa sababu dhahiri, nayo ni kuwa ameekwa mbele, ingawa Kazija hajui na nani. Daima atamchukia mwanamme kwa sababu hio. (uk. 1).

Buruhani alikuwa mstahamivu aliyeamua kwa hiari yake bila ya ushawishi wa watu kukubali kujitwika mzigo mzito wa dhamana ya kwenda kufanya ziara katika nchi ngeni bila kujali matatizo ambayo yatamkabili.” Buruhani alikuwa mtu mwenye sifa zilizotakikana zaidi. Alitokea wakati nchi yake ilipomtaka sana. Kazi yake ilikuwa kusafiri, kutalii na kuandika haaliyoyafikiri habari za mambo ya nchi ngeni aliyoyafikiri yangeweza kustawisha nchi yake ya Kusadikika (uk.19).

### 4.4.4 Fadhili na Mussa

Miongoni mwa wahusika wa Kusadikika ni Fadhili ambaye mwandishi amemuonesha kama ni kijana mwenye elimu.ambspo kwa elimu hio aliamini anatosha kuwa nyenzo muhimu itakayo msaidia katikadhamana yake ya safari ya kwenda mashariki. Kwa elimu hio aliweza kupambanua mambo mengi sana aliyokutana nayo,yale mazuri aliyoyaona aliyachukua nay ale mabaya aliyaacha.” Habari aliyorudi nayo mjumbe huyu ilikuwa sawa kabisa na elimu. Alizieleza tawala mbali mbali za nchi za mashariki kwa uwazi uliojaa ufasaha na mifano inayojulikanwa sana. (uk.19). Msanii pia amemchora Fadhili katika sifa muhimu ya

kujitolea.Kujitolea ilikuwa ni sifa muhimu sana ambayo walitakiwa kuwa nazo wajumbe wa kusadikika.

Fadhili alijua fika madhila na mashaka aliyoyapata Buruhani na faida aliyoipata ya kufungwa lakini Fadhili hakuvunjika moyo na alijitolea bila ya kuchaguliwa." Mtu mwenye sifa njema alitakiwa kujitolea mwenyewe kwa mjumbe wa mashariki kama mara ya kwanza lakini sasa mtu kama huyo alipatikana upesi sana kuliko ilivyotizamiwa. Mwandishi pia amemchora Mussa kuwa ni kijana mwenye elimu ambae amesomea udaktari baada ya fumanizi la baba yake kwa Kazija." Makusudi alipohakikisha kuwa yule aliemsimamia alikuwa mwanawe alifumbua kinywa chake kwa pupa, mu, mu, mu, alitaka kutaja jina la mwanawe (uk. 128).

Pia, mwandishi amemueleza mussa kuwa kama ni muhusika mwenye kujitolea katika maisha yake kwa maslahi ya familia na jamii yake kwa ujumla.mussa alijitolea kutoa damu yake na kumsaidia baba yake pale hali ilipozidi kuwa mbaya..., bali ni mussa ambaye ndie alietoa damu ile anayotiwa sasa. (uk. 129). Miongoni mwa tofauti ya wahusika hawa wawili Fadhili, mwandishi hakumchora kama ni kijana asiye na nidhamu mbele ya jamii yake wala mwenye kupenda starehe." uvumilivu wake ulikuwa hauna mwisho. (uk. 19).

Mwandishi amemchora mussa kuwa ni kijana mwenye tabia ya ujeuri, uhuni na mwenye kupenda starehe, mambo haya aliyarithi kwa baba yake." Saa moja nzima ilipita, mnamo saa tano na robo hivi, Kazija alimkokota mussa wake chumbani, yu chopi, kalewa analewa lewa.kitandani mussa aliendelea kuporoja (uk. 6). Mwandishi

pia amemuonesha mwisho anajirekebisha tabia zake na kuamua kusoma na kuhitimu na kuwa daktari na kusaidia jamii yake (uk. 129).

Kutokana na hoja za hapo juu ni dhahiri kuwa katika tabia za wahusika kuna mfanano na tofauti kubwa kati yao. Linapokuja suala la kulinganisha baina ya wahusika wa vitabu viwili vya utengano na kusadikika.

## 4.5 Data ya Kuonesha Tabia za Wahusika

Katika sehemu hii tunabainisha data tuliyoipata kutoka kwa wahojiwa wetu kuhusu tabia za wahusika wakuu wa riwaya teule. Majibu haya yanatokana na hojaji tuliyowapa wahojiwa hao.

## 4.6 Dhamira

Dhamira kuu ya muandishi ni ukombozi.Dhamira hii ndio kuu katika riwaya yakusadikika iliyojikita kwenye ukombozi wa kifikra na ukombozi wa kisiasa.Mwandishi mwandishi amemtumia mwandishi karama alieanzisha elimu ya sheria yenye lengo la kuwezesha wananchi ili waweze kushiriki katika mambo mbali mbali ya nchi.

### 4.6.1 Uongozimbaya

Mwandishi amedhihirisha hili kwa kuwatumia wahusika waziri Majivuno,Wafalme na madiwani na matajiri ambao ndio waliochorwa kwa taswira ya kuwa wanahaki zaidi kuliko wananchi wa kawaida.Tunapozungumzia uongozi mbaya ni hali ya utawala kutokuwajali kwa kuwasaidia wananci wa kawaida kisias,uchumi,na kijamii.(uk 7).

### 4.6.2 Uzalendo na Ujasiri

Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda nchi yake na kuipigania katika mambo mbali mbali yanayokwamisha maendeleo (pigano la kufa na kupona lilikuwa mbele yake,uk(8).

### 4.6.3 Uonevu na Ukandamizaji (Kukosekana kwa Haki)

hali ya ya kutokuthaminiwa,kupewa haki bila na kuhukumiwa bila ya kufanya kosa lolote,na wakati mwengine kutokupewa nafasi ya umuhimu katika tabaka fulani la watu:sheria za kusadikika zilikuwa haziamuru mtu yeyote kujitetea juu ya ushahidi wa mshtaki.(uk 7).miongoni mwa dhamira ni umaskini ni hali ya kutojipatiamahitaji mbali mbali ya kila siku. Dhamira nyengine ndogo ndogo katika riwaya hii tamaa iliyooneshwa kupitia salihi na majivuno,unafiki na woga wa wananchi wa kusadikika.

## 4.7 Dhamira katika Kitabu Cha Utengano

### 4.7.1 Nafasi ya Mwanamke

Huenda dhamiri au lengo la mtunzi likawa ni kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Pengine amedhamiria kuonyesha kuwa mwananamke ni sawa na mwanamme. Ni juu ya mhakiki kuona kama kweli mwanamke amechorwa kama mwenye nafasi sawa na mwanamme katika kazi hiyo. Mathalani, tuchukue jinsi Said A. Mohamed (Utengano) alivyoonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii ya wanaume wakatili kama vile Maksuudi. Mtunzi huyu amemuonyesha Maksuudi kama mwanaume mkatili anayejipenda sana, lakini hatimaye anaangushwa na mwanamke (Kazija). Vile vile twapata kwamba pale nyumbani kwa Maksuudi pametolewa amri fulani za

kufuatwana, kama vile kutawishwa kwa bintiye na bibi kutohudumiwa na mkunga. Lakini amri hii yapuuzwa na kuvunjwa kwa juhudi za mwanamke. Hivyo basi twaweza kutaja kwamba mtunzi alidhamiria kuonyesha kuwa hata mwanamke ana nafasi katika jamii ya wanaume wenye kiburi na taasubi nyingi. Lakini dhamiri hii haishikilii hadi mwisho wa hadithi kwani Kazija anatoweka hadithini naye Maimuna (ambaye ni mhusika muhimu) anaokolewa na mwanamme (Kabi)

### 4.7.2 Uongozi Mbaya

Hii ni dhamira inayojitokeza katika kazi nyingi za kifasihi, jamii nyingi za kiafrika zinaathirika na kadhia hii ya uongozi mbaya katika jamii zake. Dhana ya uongozi mbaya ni kikwazo na kipingamizi kikubwa cha maendeleo katika jamii nyingi za kiafrika. Katika riwaya ya utengeno msanii ameidhihirisha waziwazi dhana hii kwa kumchora Bwana Makusudi kama kielelezo cha uongozi mbaya katika jamii. Bwana Makusudi aliyatenda mambo mengi ambayo kwa nafasi yake katika utawala hakupaswa kuyatenda kwa raia wenziwe,alithubutu kusaliti nyumba yake, aliwanyanyasa wanawake na pia alishindwa kulipa fidia ya imani aliyopewa na raia wenziwe wakati wa kutetea uhuru wa nchi yake, uk 17. Makusudi aligombania uhuru wa nchi yake kwa tamaa kwamba wakitoka wale watu weupe,yeye atakuwa mmoja wapo atakae kamata nafasi zao.

### 4.7.3 Usaliti

Dhana ya USALITI ni dhana iliyojitokeza katika jamii nyingi katika bara la afrika, dhana hii ni moja kati ya dhana inayosababisha jamii za afrika kutokupata maendeleo. Historia inaonesha viongozi wengi wapigania uhuru wa bara la afrika wakati wa ukoloni, nchi zao zilipopata uhuru, basi viongozi hao, waliwasaliti raia

zao kama vile hawakuwa pamoja katika harakati za ukombozi mfano wa moja kwa moja ni nchi ya Zimbabwe chini ya Robert Mugabe. Katika riwaya ya utengano, msanii Said A.Mohamed amemchora Bw.Makusudi kama alama ya kiongozi msaliti kwa jamii yake, alikuwa mstari wa mbele katika harakati za ukombozi za kumuondoa mtawala mweupe, lakini kumbe alikuwa na malengo ya paukwa pakawa, alitaka nafasi ya mtawala mweupe akae yeye. Uk 17.

## 4.8 Kufanana na Kutafautiana kwa Dhamira

**Jedwali Na. 4.1: Kuonesha Tabia za Wahusika**

| WAHUSIKA | IDADI YA WAHOJIWA (50) | TABIA | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|
| MAIMUNA | 15<br>25<br>10 | Anajiamini<br>Amekiuka maadili<br>Mpole | 30<br>50<br>20 |
| MAKUSUDI | 10<br>30<br>10 | Afiriti<br>Mnyanyasaji<br>Mnafiki | 20<br>60<br>20 |
| FARASHUU | 35<br>10<br>5 | Mwenye kisasi<br>Anajiamini<br>Muwajibikaji | 70<br>20<br>10 |
| KAZIJA | 25<br>20<br>5 | Mwenye kisasi<br>Anajiamini<br>Muasharati | 50<br>40<br>10 |
| KARAMA | 37<br>10<br>6 | Mwanamapinduzi<br>Msomi<br>Mpole | 74<br>20<br>6 |
| MAJIVUNO | 38<br>11<br>1 | Mjeuri<br>Anajikweza<br>Anapenda sifa | 76<br>22<br>2 |
| BURHANI | 23<br>17<br>10 | Anapenda kujitolea<br>Mwenye subira<br>anajiamini | 46<br>34<br>20 |
| FADHILI | 25<br>20<br>5 | Anapenda kujitolea<br>Mstahamilivu | 50<br>40<br>10 |

Chanzo: Data ya Uwandani, (2016)

Jadweli hapo juu linaonesha tabia za wahusika kutoka katika riwaya zilizoteuliwa. Matokeo hayo yanatokana na majibu ya hojaji. Wahojiwa 50 walijaza hojaji hizo na kwa kutaja tabia za kila mhusuka. Mhusika Maimuna katika riwaya ya *Utengano* ameonekana na sifa au tabia ya kukiuka maadili ya jamii yake kwa 50% wakati huo huo ameonekana na tabia ya upole kwa 30% na kujiamini 20%. Hivyo, Maimuna alikuwa na 50% ya tabia nzuri na 50% ya tabia mbaya.

Muhusika Makusudi katika riwaya ya *Utengano* ameonekana na tabia asilimia 100% ameonekana na tabia mbaya. Farashuu pia wa riwaya ya *Utengano* asilimia 70% anaonekana ni mwenye kulipiza kisasi kwa yale aliotendewa na asilimia 30% anaonekana ni mwenye kujiamini na muajibikaji hivyo atakuwa ni mwenye tabia nzuri.Kazija inaonesha asilimia 50% ni mwenye kulipiza kisasi pia asilimia 40% ni mwenye kujiamini ila asilimia 10% ni muasharati ambayo si tabia nzuri.

Kuhusu muhusika Karama kati ya hojaji 50%, 74% wameonesha kuwa ni mwanamapinduzi na asilimia 20% ni msomi amma asilimia 6% ni mpole hivyo karama ni mwenye tabia nzuri. Majivuno wa riwaya ya kusadikika kati ya hojaji waliohojiwa majibu yanaoneha kuwa asilimia 76% ni mjeuri na asilimia 22% anapenda kujikweza na asilimia 2% anapenda sifa hivyo majivuno ni mwenye tabia mbaya.

Buruhani wa riwaya ya utengano majibu yanaonesha asilimia kubwa 46% inaonesha anapenda kujitolea asilimia 34% ni mwenye subra na asilimia 20% anajiamini hivyo asliimia kuwa ni mwenye kujitolea. Fadhili nae wa riwaya ya utengano majibu

yaliotolewa ni kuwa asilimia kubwa 50% wamesema ni mwenye kupenda kujitolea na asilimia 40% ni mstahamilivu na asilimia ndogo yao ni mwenye subra. Hayo ni majibu ya tabia za wahusika kama yalivyoonekanwa kwenye jadweli na jinsi ya mahojaji walivyotoa maoni yao.

## 4.9 Hitimisho

Katika sura hii tumebainisha tabia za wahusika wakuu wa riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano.* Katika riwaya zote mbili, imebainika kuwa waandishi wametumia tabia nzuri na mbaya kwa wahusika wao. Hata hivyo, ilibainika kuwa riwaya zote mbili ni matokeo ya athari ya mapokeo simulizi ya Kiafrika. Hii inatokana na watunzi kuathiriwa na mapokeo simulizi ya visakale vya watu wa pwani. Vilevile tumelinganisha na kutafautisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano*. Kwa ujumla, katika sura hii, utafiti ulibaini kuwa riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano* zinafanana sambamba na kutofautiana. Vile vile utafiti umegundua kuwa Shaaban Robert amesawiri tabia za wahusika wa riwaya yake zinazolingana na majina yao. Kwa mfano: Majivuno na Karama. Hivyo tunaweza kuchukulia kuwa, huu ndio mtindo wa watunzi katika uandishi wa kazi za fasihi.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ambayo ndio ya mwisho inahusu muhutasari wa mjadala wa utafiti, kujibu maswali ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo kuhusu kufanya utafiti zaidi. Pia, sura hii inatathimini ya jumla ya utafiti, kuanzia lengo kuu, malengo mahususi na maswali ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Mjadala

Katika sehemu hii tunaelezea muhutasari wa mjadala wa utafiti kuanzia sura ya kwanza mpaka sura ya tano. Katika kila sura tumeanza na utangulizi na kuendelea na mjadala na kumalizia kwa hitimisho la sura inayohusika. Kwa hiyo, tasnifu hii ina jumla ya sura tano zilizopangwa kwa mujibu wa mwongozo na taratibu za uandishi wa ripoti ya utafiti za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Tukianza na sura ya kwanza, hii inahusu utangulizi wa jumla ambao unatoa maelezo ya awali kuhusu mada ya utafiti pamoja na kueleza umuhimu wa kutafiti mada hii. Sura hii imeanza kwa kueleza taarifa za awali za utafiti ambazo ni pamoja na usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na mpangilio wa tasnifu.

Aidha, sura ya pili inaeleza mambo matatu muhimu ambayo ni pamoja na mapitio ya kazi tangulizi, kiunzi cha nadharia ya utafiti pamoja pengo la utafiti. Katika mapitio ya kazi tangulizi, sura hii imefafanua kazi tangulizi mbalimbali zinazohusiana na

mada ya utafiti ambazo mtafiti alizipitia. Madhumuni ya kupitia kazi tangulizi hizo ni kubaini pengo la utafiti ikiwa ni pamoja na kupata mwanga wa masuala muhimu ya kufanya ili kufikia malengo ya utafiti.

Pia, sura ya tatu inaeleza mbinu za utafiti ambapo imeanza kufafanua mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Kwa ujumla, sura hii imeeleza namna taarifa za utafiti huu zilivyokusanywa na kuchambuliwa hadi kuandikwa ripoti hii ya utafiti. Taarifa za utafiti zimekusanywa kwa mbinu kuu tatu za ukusanyaji wa data. Mbinu hizo ni dodoso na mapitio ya maandiko. Pia sura hii imeeleza mbinu zilizotumika katika mchakato wa uteuzi wa sampuli na mbinu zilizotumika katika uchambuzi wa data za utafiti.

Vilevile, sura ya nne inaeleza kuhusu uwasilishaji na uchambuzi wa data. Kwa ujumla sura hii ndio kiini cha utafiti kwa sababu data zote zilizokusanywa maktabani na uwandani zimewasilishwa na kuchambuliwa katika sehemu hii. Uchambuzi wa data za utafiti umefanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ambapo mbinu za uchambuzi wa kifasihi zimetumika. Kwa hakika sura hii imebainisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu ulinganishi wa tabia za wahusika wakuu katika riwaya ya Kiswahili.

Halikadhalika, sura ya tano inahusu muhutasari wa mjadala wa utafiti, hitimisho na mapendekezo juu ya utafiti zaidi. Pia, katika kipengele cha muhutasari tumejaribu kujibu maswali ya utafiti na kubainisha mchango wa utafiti. Mwisho, tumetoa maoni baada ya kukamilisha utafiti ili kujenga taaluma ya fasihi kwa kufanyika utafiti zaidi.

### 5.2.1 Kujibu Maswali ya Utafiti

Kama tulivyoeleza hapo awali kuwa utafiti huu ulikusudia kulinganisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* ili kubaini namna waandishi wanavyoibua dhamira kupitia tabia wanazowapa wahusika hao. Hivyo basi, katika mchakato wa kulinganisha na kujadili tabia za wahusika wakuu katika Riwaya ya *Kusadikika* na *Utengano,* pia utafiti huu ulijaribu kujibu maswali ya utafiti (taz. sehemu ya 1.5) ambayo yanatokana na malengo mahususi ya utafiti huu. Kwa ujumla, maswali hayo yalikuwa matatu kama ifuatavyo:

Swali la kwanza lilikuwa linauliza: *Kwa ufupi riwaya za Kusadikika na Utengano zinaeleza nini?* Kama ilivyokwishabainishwa, katika sehemu ya uchambuzi wa data (taz. Sura ya nne) riwaya zote mbili zinazungumzia ujenzi wa jamii mpya. Riwaya ya *Kusadikika* inasimulia uovu wa viongozi kwa raia jinsi viongozi hao walivyokithirisha dhulma, ukandamizi, uonevu na udhalilishaji. Ingawa jamii nayo inadai mabadiliko kwa nguvu zote bila kujali ubaya wa viongozi wao. Halikadhali, riwaya ya *Utengano* inabainisha udhulma, ukandamizaji na uonevu uliotawala katika jamii hasa baada ya kuanguka kwa utawala wa kikoloni. Kwa ujumla, riwaya zote mbili zimejaribu kufichua maovu yaliyotawala katika nchi za Afrika wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Waandishi wa riwaya hizo wanataka haki isimame katika ujenzi wa jamii mpya.

Swali la pili la utafiti huu lilitakakujua: *Kuna wahusika gani wakuu katika riwaya za Kusadikika na Utengano na wamebeba tabia gani?* Kwa mujibu wa data ya utafiti, tumebaini kuwa kila riwaya ina wahusika wa aina mbili ambao ni wahusika wakuu na wahusika wasaidizi au wahusika wadogo. Kwa hiyo, kutoka kila riwaya

tumechukua wahusika wanne kubainisha tabia za wahusika katika riwaya inayohusika. Katika riwaya ya *Kusadikika*, kwa mfano, tumebaina wahusika kama vile Karama, Majivuno, Burhani na Fadhili. Katika riwaya ya *Utengano* tumewatumia wahusika kama vile, Makusudi, Maimuna, Farashuu na Kazija. Tabia za wahusika zilizobainishwa ni za aina mbili; yaani tabia chanya na hasi. Kwa upande wa tabia chanya zimeinishwa tabia kama vile busara, hekima, uzalendo, uwajibikaji, kujiamini na kadhalika. Ama kuhusu tabia hasi, tumebaini tabia kama vile, udhalimu, unafiki, ukandamizaji, jeuri, uasharati na majivuno.

Kwa hakika, tabia zote hasi imekuwa ni kikwazo katika ujenzi wa jamii mpya yenye utawala wa haki na sheria. Tumeweza kuona katika riwaya ya *Kusadikika* jinsi utawala wa Wasadiki kupitia waziri mkuu Majivuno ulivyokandamizi juhudi za wananchi waliojitolea kwa uzalendo wao kwenda nchi za mbali kutafuta maendeleo ya nchi yao. Lakini kutokana na kiburi, jeuri na kujidai kwa baadhi ya viongozi wanaowakilishwa na Majivuno, wananchi hao juhudi zao hazikuthaminiwa badala yake walivunjiwa kadri na kuishia mashtaka na kifungo. Aidha, katika riwaya ya *Utengano* tunaona jinsi dhulma na unyanyasaji wa wanawake zinavyotawala kutokana kukosekana kwa misingi ya haki na utawala wa sheria. Bila shaka hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli bila haki na sheria kusimama katika nchi zetu.

Kwa hiyo, katika riwaya teule tunaona kwamba waandishi wa riwaya zote mbili wanaonekana kuwa wanasawiri tabia mahususi wa wahusika wao ili waweze kuibua dhamira walizozikusudia katika kazi zao hizo. Matendo ya wahusika ambayo husimama kama tabia zao ndio yanayoibua maudhui ya kazi ya fasihi inayohusika. Waandishi husawiri majina yanayo inaendana na tabia za wahusika. Kwa mfano,

Majivuno wa *Kusadikika,* jina linaenda sambamba na tabia zake. Aidha, Makusudi wa *Utengano* jina lake linaenda sambamba na tabia za bwana huyu kufanya vitendo vya dhulma na ukandamizaji kwa makusudi.

Swali la tatu lilitaka kubaini: *Tabia za wahusika wakuu wa riwaya za Kusadikika na Utengano zinafanana na kutofautianaje?* Matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kwamba kuna kulingana na kutofautiana kwa tabia za wahusika katika riwaya mbili hizo. Tukianza tabia zinazofanana kwa mfano, wahusika kama vile Karama wa *Kusadikika* na Farashuu wa *Utengano* wanafanana katika tabia zao chanya kama vile uzalendo, kujiamini, kujitolea kwa ajili ya nchi zao na uwajibikaji. Pia, wahusika kama vile Majivuno wa *Kusadikika* na Makusudi wa *Utengano* wanafanana katika uwakilishi wa wahusika wenye tabia hasi. Wahusika hao wanaonekana wenye tabia za uafiriti, wakandamizaji, wanafiki, kiburi na jeuri.

Aidha, kwa upande wa kutofautiana kwa tabia za wahusika wa riwaya za *Kusadikika* na *Utengano* data yetu inabainisha kuwa katika riwaya ya *Kusadikika* hakuna mhusika mwanamke ambaye anafanya uasharati kama tunavyomuona Maimuna katika riwaya ya *Utengano.* Tofauti za tabia za wahusika kutoka riwaya moja na nyingine mara nyingi huchangiwa na dhamira za mwandishi kuhusu kazi yake na ujumbe aliokusudia kuutoa kwa jamii inayohusika. Katika riwaya ya *Kusadikika* kwa mfano, mwandishi Shabaan Robert alidhamiria kufichua maovu yaliyofanywa na viongozi au watawala wa nchi kwa kuwakandamizi wengine bila kujali utawala wa haki na sheria. Said Ahmed Mohamed katika riwaya yake ya *Utengano* kwa Upande wake alikusudia kubainisha ukandamizaji wa kijinsia unaofanywa na wanaume

katika jamii za Kiafrika. Kutofautiana kwa dhamira kuu za riwaya hizi kumesababisha pia wahusika waweze kutofautiana kitabia.

### 5.2.2 Mchango wa Utafiti

Kwa ujumla utafiti huu una mchango mmojawapo katika taaluma ya fasihi hususani katika utanzu wa riwaya za Kiswahili kwa jamii ya Watanzania. Mchango huo unajibainisha katika mambo yafuatayo. Mosi, unatoa mchango wa kubainisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya za Kiswahili na jinsi waandishi wanavyozitumia tabia hizo katika kuibua dhamira mbalimbali za kazi zao. Utafiti umeweza kuwaweka bayana wahusika wakuu katika riwaya teule.

Pili, utafiti huu umeweza kulinganisha tabia za wahusika zilizobainishwa na mwandishi mmoja na mwingine. Katika ulinganisho huo, utafiti huu umeweza kugundua kufanana kwa baadhi ya tabia na kutofautiana kwa tabia nyingine. Tatu, utafiti huu unachangia kubainisha wasomaji wa kazi za fasihi kuwa mwandishi mmoja na mwingine hufanana na kutofautia katika kusawiri tabia za wahusika wakuu kulingana na dhamira za kazi yake alizodhamiria kufikisha ujumbe kwa jamii inayohusika.

Sambamba na hayo, utafiti huu umegundua kuwa wahusika ni watu au viumbe wengine ambao msanii mwenyewe huwabuni kutokana na maisha ya jamii yake kulingana na kile anachotaka kukifafanua kwa jamii hiyo. Kwa hivyo, katika kazi yoyote ya fasihi wahusika wanaweza kuwa watu, wanyama au vitu vingine ambavyo vitabuniwa na mwandishi. Msisitizo unaouweka ni kuwa tabia na matendo ya wahusika hao ambao hubuniwa na mwandishi ndio ambao huwatumia kisanaa ili waweze kuwakilisha nyanja mbalimbali za maisha ya jamii. Waandishi huwasawiri

wahusika kwa kuwapa sifa pambanuzi ambazo huakisi dhamira maalumu zinazokusudiwa na mwandishi katika kufikisha ujumbe fulani kwa jamii inayohusika.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu umelinganisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni riwaya za *Kusadikika* iliyoandikwa na Shaaban Robert na *Utengeno* iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Lengo kuu lilikuwa ni kulinganisha tabia za wahusika wakuu katika riwaya teule ili kubaini namna wanavyojenga dhamira. Utafiti huu umebainisha kuwa tabia za wahusika zinazobuniwa na mwandishi zinatakiwa kwa kiasi kikubwa zilenge uhalisi wa mambo yaliyomo katika jamii.

Kwa kuhitimisha, utafiti huu umeweza kukamilisha malengo mahususi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, riwaya hizi mbili zinabainisha tabia za wahusika wakuu ambazo zinasawiri dhamira mbalimbali ambazo zinauhalisia katika maisha ya siku hizi japokuwa riwaya zenyewe zilitungwa miaka mingi iliyopita. Katika riwaya ya *Utengano* tabia za wahusika zinaibua dhamira mbalimbali kama vile, matabaka katika jamii, ukahaba, ubakaji, ndoa za kulazimishwa, mapenzi, dhulma na ukarimu.

Katika riwaya ya *Kusadikika* pia, tabia za wahusika zinaibua dhamira kama vile busara na hekima, umuhimu wa elimu, umasikini, utamaduni na mabadiliko yake, ukombozi katika jamii na ukandamizaji wa haki. Kwa ujumla dhamira hizo wandishi wameziibua kupitia tabia za wahusika ambao wamewabuni katika kazi zao zinaleta uhalisia wa mambo yalivyo katika jamii. Kwa mfano, masuala ya kuwepo matabaka na umasikini katika jamii ni matatizo kubwa katika jamii ya leo ikilinganishwa na jamii za kipindi ambacho riwaya hizo zilipoandikwa. Aidha, ukandamizaji wa haki

za wanyonge na kukosekana kwa utawala unaosimamia haki na sheri ni matatizo sugu katika jamii za leo.

## 5.4 Mapendekezo

Bila shaka, hakuna utafiti ambao unaweza kuchukuliwa kuwa umekamisha kila kitu katika eneo ulilolichunguza. Kwa maana hiyo ni dhahiri kwamba utafiti huu haujamaliza kila kitu katika eneo ulilolitafiti. Kwa hiyo inawezekana kwamba yapo maeneo mengine ambayo hayajashughulikiwa kama inavyostahili. Kwa sababu hiyo, utafiti zaidi unaweza kuhitajika kukutafiti tabia za wahusika wakuu katika kazi nyingine za fasihi andishi kama vile tamthiliya, riwaya nyingine na kadhalika.

Kwa vile wahusika ndio wanaotawala kazi ya fasihi, tunapendekeza kwa waandishi kuwa wa kazi za fasihi wabuni wahusika ambao wanafichua kuonesha matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii. Hali hii inaweza kuwasaidia wasomaji wa kazi za fasihi kupata mafunzo ya kutosha juu ya mambo yaliyomo katika jamii zao. Hivyo basi, msomaji anaweza akaelimika kutokana na mafunzo atakayopata katika kazi ya fasihi na hatimaye kuweza kujiepusha na maovu yanayotendeka ndani ya jamii. Aidha, tunapendekeza wa watafiti wengine wachunguze tabia na matendo ya wahusika wakuu kwa kulinganisha yanayoandikwa katika kazi za fasihi na uhalisia wake katika jamii. Kwa sababu kuna baadhi ya tabia za wahusika halielezwi kwa uhalisia wake kama zinavyochukuliwa katika jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Utengano* tunamuona muhusika Kazija amesawiri ikiwa na tabia ya uasharati lakini hali inayoelezwa kwenye kazi ya fasihi inaweza kutofautiana na uhalisia wa suala hili katika jamii.

## MAREJEO

Ameir. S. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi Zanzibar*. Zanzibar: Taasisi ya Lugha za Kigeni.

Bakwasegha, C. (1982), *Profiles of Urban Prostitution: A case study from Uganda.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Buliba na wenzake .2014. *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Dar es Salaam: Serengeti Educational Publisher limited.

Cohen, L. Manion, L. na Morrison, K. (2000). *Research Methods in Education*. New York: Routledge Falmer.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Enon, J. C. (1998), *Education Research, Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University.

Gibbe, A. G. (1978). "*Dhima ya Mhakiki ", katika: Mulika.* Dar es Salaam: TUKI.

Gibbe, A. G. (1978). *"Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960-1977" katika. Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI. Juzuu la 48/1.

Hegel, G. W. F. (1971). *Introduction to Aesthetics.* Oxford: Clarendon.

Kezilahabi, E. (1975). Shaaban Robert: Mwandishi wa Riwaya. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (2006). *Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati*. Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI 2005. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, K. na Kisovi, C. N. M. (2005), *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Literature Bureau.

Kombo, D. K. na Tromp, D. L. A. (2006), *Proposal and Thesis Writting: An Introduction.* Nairobi: Pouliness Publications.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques,* New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology, Methods and Techniques*. New York: New Age International (P) Ltd.

Libiu, O. S (2012), “Riwaya Mpya ya Kiswahili na Masuluhisho ya Changamoto za Utandawazi”. Tasnifu ya M. A Kiswahili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Lyatuu, J. (2011). “Usawiri wa Mwanamke Katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Mwandishi wa Kike na wa Kiume Uchunguzi Katika Riwaya Teule”. Tasnifu ya M. A. Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mabala, R. S. (1993). *“Mchango wa Waandishi wa Riwaya”, ktk: Fasihi, Uandishi na Uchapishaji.* Dar es Salaam: DUP.

Madumulla, J. S. (1988). *“Riwaya ya Kiswahili (Tanzania) katika Miaka ya Themanini”, katika Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.

Madumulla, J. S. (1987). *“Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania”, ktk:* Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.

Madumulla, J. S. (1993). *“Mwandishi wa Riwaya: Ukweli kuhusu Maisha”, katika:* Mulika. Dar es Salaam: TUKI.

Maganga M. A (1996). *Maisha ya shaaban Robert na mawazo yake katika uchambuzi wa maandishi,* Oxford: Oxford University Press.

Khamis, M. H. (2007). Taswira za Wahusika Wakuu katika Riwaya Tano za Shaaban Robert. Tasnifu ya Shahada ya kwanza, Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA. Zanzibar, Tanzania.

Mazingwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili*, Paramilo BPN.

Mhilu, G, Nyangwine, N. na Kanyuma, Y. (2013). *TAHAKIKI: Vitabu Teule vya Fasihi, Kidato cha 3 na 4.*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mlacha S.A.K. na Madumla J.S. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam University Press.

Mlacha S. A. K. (1985). *Wahusika katika riwaya za Kiswahili*, Taasisi ya Kiswahili ya uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam.

Mlacha, S. A. K. (1993). *Kiswahili Novels and Society*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S. A. K. (1984). *"Riwaya za Visiwani (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya", katika Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.

Mligo, E. S. (2012), *Jifunze Utafiti. Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering EGYS.

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano.* Nairobi*:* Longhorn Publishers.

Msokile, M. (1993). *Uchambuzi na uhakiki wa riwaya kidato cha nne*, Dar es Salaam: University Press Dar es salaam.

Mulokozi, M. M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mutembei, A. K. (2000), *"Fasihi ya Kitaifa na Fasihi ya Kiswahili ni Dhana Ileile?" Katika Mulika*. Dar es Salaam: TUKI

Nassor, G. H. M. na Hamad, A. K. H. (2006), *Wahusika na matumizi ya lugha katika riwaya M. S. Abdullah*. Dar es Salaam: DUP.

Nguma, N. (2001). Taswira ya Mwanamke Jinsi Ilivyochorwa Katika Riwaya ya Kezilahabi. (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa) Chuo Kikuu cha D' Salaam.

Njogu, K na Chimerah, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College

Padgett, D. (2002). *Qualitative Methods in Social Work Research: Challenges and Rewards*. London: Sage Publications Inc.

Robert, S. (1951) *Kusadikika*, Nelson, Nairobi

Said, A. M.(1984). *Mwongozo wa Utengano,* Nairobi: Heinemann. Educational books (E.Africa) Ltd,

Senkoro, F. E. M. K. (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *"Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili", katika: Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: JKF.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wellek, R. (1961). *"The Concept of Realism in Literary Scholarship".* Neophilologus. London: J Cape

# KIAMBATANISHO

**Kiambatanisho 1: Idadi ya Watafitiewa**

| WALIOTAFITIWA | WANAWAKE | WANAUME | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Wanaosoma somo la Kiswahili Fasihi Shahada ya kwanza | 30 | 20 | 50 |

**MASWALI KWA WATAFITIWA WA CHUO CHA SUZA WA SHAHADA YA KWANZA**

Jina la mwalimu ………………………………………………………………………

Jinsia: Mke ☐ Mume ☐

Shule au Chuo anachosomesha

Jaza hapa ……………………………………………………………………………

Darasa langapi?

Jaza hapa …………………………….. Mwaka………………………………..

1) Jee umewahi kusoma riwaya ya kusadikika ya shaaban Robert na utengano ya Said Ahmed?

Ndio au hapana ………………………………………………………………………

2) Bainisha wahusika wakuu wa riwayazote mbili

Jaza hapa ………………………………………………………………………………….

3) taja tabia tatu za wahusika wafuatao wa riwaya ya Utengano ya Said A. Mohamed

a) Maimuna

i) ……………………………………..

ii) ……………………………………..

iii) ……………………………………..

b) Makusudi

i) ………………………………………

ii) ………………………………………

iii) ………………………………………

c) Farashuu

i) ……………………………………

ii) ……………………………………

iii) ……………………………………

d) Kazija

i) …………………………………….

ii) …………………………………….

iii) …………………………………….

4) Taja tabia za wahusika wafuatao kutoka katika riwaya ya Kusadikika ya Shaaban Robert

a) Karama

i) ………………………………………

ii) ……………………………………..

iii) ……………………………………..

b) Majivuno

i) ………………………………………

ii) ………………………………………

iii) ………………………………………

c) Burhani

i) ………………………………………….

ii) ………………………………………….

iii) ………………………………………….

d) Fadhili

i) ……………………………………......

ii) …………………………………………

iii) …………………………………………

5) Kutokana na alivyowachora wahusika hao, unafikiri kuna sababu gani kwa Shaaban

Robart na Said Ahmed kuwapa majina ya Karama, muhusika mkuu wa Kusadikika na makusudi wa utengano?

Jaza hapa

…………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………….